SUPA JACKPOT
TZS. 1,065,505,647
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

UKURASA 3



**DART** yatoa mabasi maalum kwa wanafunzi tu




UKURASA 11

Nipashe
Alhamisi Januari 12, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581188
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo.


Marehemu Nelson Mollel

# Kijana auawa kwa madai kuchapwa fimbo 280

**NI** adhabu ya kimila, baba asakwa... *Endelea ukurasa 2*

## Watoto 70 walivyokeketwa, ngariba, wazazi matatani

UKURASA 2



## Dk. Shein: Mapinduzi yalianza na hoteli mbili, leo ziko 600

UKURASA 12

Mwonekano wa Hoteli ya Kilindini iliyoko Pwani Mchangani, Wilaya ya Kaskazini "A", Zanzibar, baada ya kufunguliwa rasmi na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (hayupo pichani), ikiwa ni sehemu ya shamrashamra kuelekea maadhimisho ya Miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar jana. **PICHA: OWM**

**MICHEZO** FEI TOTO AGOMA KURUDI JANGWANI UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Aliyekuwa Meneja Matangazo na Miradi wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Angel Navuri, akimlisha keki Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe katika chumba cha habari cha TGL, Mikocheni Viwandani, Dar es Salaam jana, kama ishara ya kuwaaga wafanyakazi wenzake baada ya kumaliza mkataba wake. **PICHA: JOHN BADI**

# Kijana auawa madai kuchapwa viboko 280

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

NELSON Mollel (32), Mkazi wa Sanawari, Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, amepoteza maisha kwa madai ya kuchapwa viboko 280 na kumwagiwa tindikali kiunoni na viongozi rika wa kimila, akituhumiwa kumtukana mama yake mzazi matusi ya nguoni.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Richard Ruyango, alithibitisha kupokea taarifa za tukio hilo na kusema kilichofanyika sio adhabu, bali mauaji ya kikatili.

Kutokana na tukio hilo, Ruyango, alisema vyombo vya usalama viko kazini na baada ya kukamilisha kazi yake, serikali itachukua hatua kali kwa waliohusika na mauaji ya kijana huyo.

"Tunaufahamu utaratibu wa adhabu ya fimbo 70, lakini kilichofanyika ni zaidi ya adhabu. Kilichofanyika sio adhabu, bali ni tukio la mauaji," alisema.

Akizungumza na Nipashe kuhusu tukio hilo, Jackline Mollel, dada wa marehemu, alisema mdogo wake kabla ya umauti kumkuta, alichapwa fimbo 280, badala ya 70 zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria ya mila ya kabila la Kimasai.

"Lakini baada ya kumchapa fimbo hizi 280, walimwagia tindi kali eneo la kiunoni na kupoteza maisha. Mila zetu zinataka mtu mwenye utovu wa nidhamu, achapwe fimbo 70, lakini wao walipitiliza," alidai.

Alisema hawapingi adhabu aliyopewa mdogo wake na baba yao mdogo, Abel Mboya, kwa kushirikiana na watu wengine 10, kumchapa fimbo hizo bila kuangalia afya ya mhusika huyo.

"Sisi hatukatai ndugu yetu kuchapwa, maana ni mila na desturi zetu sisi Wamasai, lakini wamezidisha na wamemchapa kwa sifa na wamemvunja mbavu, miguu, mikono na kummwagia tindikali chini ya kiuno," alisema Jackline.

Akizungumzia tukio hilo, mama mzazi wa marehemu, Janeth Kimario, alikiri mtoto wake kumtukana matusi hayo ya nguoni, Januari mosi, mwaka huu.

"Baada ya kunitukana, nilimwambia baba yake mdogo, ambaye alimwita na kumpeleka porini na nikajua anamchapa fimbo 70 ambazo mila zetu zinataka.

"Adhabu aliyopewa mwanangu ni kubwa, japo alistahili kuchapwa kufundishwa adabu, lakini hata hivyo, hawakuniambia kama watampa adhabu kubwa hivyo hadi kupoteza maisha."

Kwa mujibu wa mama huyo, baba mdogo wa marehemu, alishawahi kumpiga yeye na kumvunja kidole na kisha kumwambia bado atafanya mauaji kwa wengine iwe fundisho.

***Imeandikwa na Cynthia Mwilolezi na Tumaini Mafie (ARUSHA)**

# Watoto 70 walivyokeketwa, ngariba na wazazi kitanzini

**Na Vitus Audax,** MARA

SERIKALI mkoani Mara imeliamuru Jeshi la Polisi mkoa wa kipolisi Tarime-Rorya kuwakamata ngariba, viongozi wa vijiji, mitaa na wazazi wa watoto 70 waliokeketwa baada ya kurudi nyumbani katika kipindi cha likizo.

Wasichana hao walikuwa wakiishi nyumba salama zilizojengwa na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuepuka kukeketwa kipindi cha Desemba.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Jenerali Suleiman Mzee, wakati wa ziara yake ya kikazi katika vituo vinavyohifadhi watoto hao.

Alibainisha kuwa ratiba ya ukeketaji hufanyika Desemba ndiyo maana watoto hukimbilia vyumba salama, lakini wazee hao walibadili ratiba na kuongeza muda ili kuwafanyia tohara watoto baada ya kurejeshwa nyumbani kipindi cha likizo kutoka kwenye nyumba hizo.

Mzee alisema baadhi ya watoto hao walikimbia kukeketwa na walikuwa wakipatiwa elimu ya kupinga vitendo vya ukeketaji wakati wa likizo ya mwezi Desemba, 2022 katika moja ya shirika lisilo la kiserikali lililoko Kijiji cha Masanga Kata ya Gorong'a wilayani Tarime.

Alisema siku tatu baada ya watoto hao kutoka katika nyumba salama na kurejea kwao, wazazi wao waliwapeleka kukeketwa.

"Nimeshakabidhi orodha ya majina ya watoto 70 wote waliokuwapo katika kituo hicho kuhakikisha wazazi wao pamoja na viongozi wanawakamata na kufikishwa mahakamani," alisema Suleiman.

Alisema serikali haiwezi kujinasibu inapambana na vita dhidi ya vitendo hivyo ilhali bado kuna wazazi wanaoendelea navyo.

Vilevile, alitaka viongozi kujitathmini katika utendaji wao huku akiwasisitiza kuwachukulia hatua wahusika wa vitendo hivyo ili kumaliza ukatili wa wanawake na watoto mkoani humo.

Mzee alisema, katika msimu huo wa ukeketaji mkoa huo umewapokea watoto 750 waliokimbia kukeketwa na kuahidi kutoa Shilingi milioni tano kwa ajili ya kuwasaidia watoto ambao bado wapo kituoni hapo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Masurura, Yusuf Chacha, aliwashauri wananchi waachane na mila potofu na badala yake waendelee na wakati wa sasa ambao mila hiyo imeshapitwa.

Aliwataka viongozi wa kimila na wengine kuingilia kati jambo hilo ili kuwe na kauli moja katika kupinga ukatili huo dhidi ya watoto.

Baadhi ya wananchi akiwamo, Yuritha Albert, alikemea hali ya ongezeko la vitendo hivyo vinavyokiuka haki za watoto huku wakiiomba serikali kuongeza juhudi za kupambana na vitendo hivyo.

Mwishoni mwa mwaka jana katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili, Shirika lisilo la Kiserikali Hope for Girls and Women, lilizindua filamu iitwayo 'In the Name of Your Daughter' (Kwa jina la Binti yako) ikionyesha wasichana wanavyokimbia kwenda nyumba salama na wanavyorudishwa kwenye familia zao.

Mkurugenzi wa nyumba hiyo, Rhobi Samuel, alisema filamu hiyo ilifanyika mwaka 2018 na ndani ya siku 11 walipokea wasichana zaidi ya 271 waliotaka kukeketwa, na ilipofika Januari waliwarudisha kwa familia zao, lakini 70 walikataliwa na kuungana na wenzao wengine kulelewa kituoni.

"Bado familia zinakumbatia mila hii ya kikatili, wanahusisha wazee wa kimila ambao ndiyo hupanga tarehe ya ukeketaji na kuchagua ngariba, watoto wanatishiwa kwamba wakikataa watakufa au wazazi wao watakufa, wanaathirika kisaikolojia, mtoto wa kike anatakiwa aolewe ili ng'ombe za mahari ya kaka yake zipatikane," alisema.

Ofisa Programu, Emmanuel Goodluck alisema tatizo kubwa vijana wanaamini ukeketaji unawapatia kipato kama kushona mavazi ya sherehe, kazi za muda mfupi na huduma nyingine, wanapata fedha na msichana akikeketwa watapata ng'ombe wa kuolea.

Askari Polisi wa Dawati la Jinsia, Kituo cha Polisi Mugumu, ambaye alishiriki kwenye filamu hiyo, Sijali Nyambuche, alisema wanawasaidia waathirika ikiwamo kuwafikisha mahakamani watuhumiwa, lakini bado tatizo ni kubwa kwa kuwa licha ya hatua kali bado wameendeleza mila hiyo.

Hivi karibuni, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Jinsia na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliwataka wanawake kufichua ukatili unaoendelea kwenye jamii, kujadili kwa kina kwenye vikao mbalimbali na wasikubali kikao kisicho na ajenda ya kuweka mikakati kukabili matukio hayo.

Aidha, alisema ni muhimu jamii zinazokeketa kuacha mara moja kwa kuwa serikali iko macho muda wote na hatua zitachukuliwa kwa wanaohusika.

HABARI KITAIFA

## Mwanafunzi darasa la 6 akutwa kajinyonga

**Na Boniface Gideon,** TANGA

MWANAFUNZI wa darasa la sita Shule ya Msingi Tewe, Tarafa ya Maramba wilayani Mkinga, Shabani Said (12), amekutwa amejinyonga kwa kutumia kanga ya mama yake.

Mwanafunzi huyo mkazi wa mtaa wa Mtambo wa Lami, Kata ya Mzizima, Amboni alichukua uamuzi huo siku chache akitarajiwa kurejea shuleni baada ya kununuliwa mahitaji yote muhimu.

Tukio hilo linadaiwa kutokea Januari 10, mwaka huu, majira ya saa saba mchana, baada ya mama yake kuingia ndani na kukuta kijana huyo amejinyonga nyumbani kwao.

Hata hivyo, hakuacha ujumbe wowote kuhusiana na tukio hilo.

Mjomba wa marehemu, Bakari Abdalah, akizungumza na waandishi wa habari, alisema hajui sababu za mwanawe kuchukua uamuzi wa kujinyonga.

"Familia hatujafahamu sababu za mtoto wetu kujinyonga, pia hajaacha ujumbe wowote, alikuwa ameandaliwa maandalizi yote ya shule na alipaswa kuondoka leo (jana) lakini ilipofika saa saba mchana mama yake mzazi alipoingia ndani alimkuta akiwa ananing'inia chumbani kwake," alibainisha.

Kwa mujibu wa mjomba, mtoto wao hakuwa na matatizo yoyote ya akili wala mgogoro na wanafamilia.

"Mtoto alikuwa anaishi Maramba na mama yake wa kambo na hapa alikuja likizo kwa mama yake mzazi na hatujawahi kusikia jambo lolote baya kutoka kwa mzazi wa pili, hivyo imetushangaza sana kuona mtoto wetu kujinyonga," alisema kwa masikitiko.

Baadhi ya majirani walisema mtoto huyo hakuwahi kuonyesha tabia yoyote mbaya na alikuwa mchangamfu muda wote.

"Majirani tumeshangazwa kuona mtoto huyu akiwa amejinyonga, sisi tulikuwa nae leo hii hadi mchana alikuwa anacheza na wenzake na kiukweli imetuhuzunisha sana suala la mtoto huyu kujinyonga," alisema Juma Kassim.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Henry Mwaibambe, akizungumza na Nipashe kwa simu alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

# DART yaongeza mabasi maalum kusaidia wanafunzi

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), imelazimika kuongeza mabasi manne kwa ajili ya kubeba wanafunzi wa shule za msingi na sekondari jijini Dar es Salaam kuwahi shuleni na kurejea nyumbani.

DART imesema iliamua kuja na mpango huo kama sehemu ya kuunga mkono sera ya elimu bure, ambayo imesababisha ongezeko kubwa la wanafunzi wa shule za msingi na za sekondari.

Mabasi hayo yanasafirisha wanafunzi hao kuanzia majira ya saa 12 kamili na saa 12.20 asubuhi mawili yakitokea Kimara kwenda Kivukoni na mawili yakitokea Kimara kuelekea Gerezani.

Mkurugenzi wa Uendeshaji na Usimamizi wa Miundombinu wa Wakala, Dk. Philemon Mzee, alisema hayo alipozungumza na gazeti hili kuhusu mkakati huo wa kusaidia wanafunzi na makundi maalum.

Dk. Mzee alisema mabasi hayo hutoa huduma hiyo pia jioni wanafunzi wanaporudi nyumbani kutoka Kivukoni kwenda Kimara kuanzia saa 10:30 na saa 11:00 na kutoka Gerezani kwenda Kimara.

Alisema huduma hiyo imewasaidia wanafunzi wengi kuwahi shuleni na kurudi nyumbani mapema bila usumbufu waliokuwa wakiupata kwenye daladala.

"Tulianza na mabasi mawili, lakini kutokana na mwitikio kuwa mkubwa tumeongeza yawe manne na ni yale marefu yenye mita 18 ambayo yanabeba watu wazima 150," alisema Dk. Mzee.

Alisema kwa sasa wanafunzi wa shule sita za Kimara, saba za Kivukoni, 14 za Gerezani na saba za Ubungo wananufaika na mabasi hayo.

"Huduma hii imeanza baada ya kufanya utafiti kwa shule zilizoko jirani na huduma yetu ya mabasi yaendayo haraka kwa kuanza na shule chache za jirani za Muhimbili, Olimpio, Gerezani na Mchikichini."

Alisema DART pia inatoa kipaumbele kwa makundi maalum ya wazee, wenye ulemavu na wajawazito kwa kuwa wamewawekea mazingira mazuri kuhakikisha wanakuwa wa kwanza kuingia kwenye usafiri huo nyakati zote.

"Hata wakikuta watu wamekaa kwenye viti ndani ya mabasi kwa wale abiria wanaopandia njiani ni sharti kwamba wapishwe wakae na hilo limekuwa likitekelezwa vizuri tu na tunawashukuru abiria wetu ni waelewa," alisema.

Derrick Mwambe, anayesoma Shule ya Msingi Mtendeni, alisema usafiri huo umekuwa neema kwao kwa kuwa wanafika shuleni kwa wakati na bila usumbufu.

Alisema wanafunzi walikuwa wakinyanyasika kwa kukataliwa kwenye daladala na kuwasababishia kuchelewa kufika shuleni na kurudi nyumbani wakati wa jioni.

"Nimefurahi usafiri huu raha sana, tuko wenyewe ndani ya mabasi hatubanani na hata tukilipa nauli tunarudishiwa chenji kwa urahisi tofauti na kwenye daladala," alisema.

Arodia John wa Shule ya Msingi Mnazi Mmoja, alisema usafiri huo umewafanya kufurahia shule kwa kuwa mazingira ya usafiri ni rafiki na hawanyanyasiki kama zamani.

"Tumekuwa tukisukumwa sukumwa tusiingie kwenye mabasi ya daladala na wakati mwingine tunakaa muda mrefu vituoni, lakini kwa utaratibu wa mabasi haya tunapanda wenyewe na kwa utaratibu bila kusukumana," alisema.

Mmoja wa wazazi ambaye mtoto wake anasoma Shule ya Msingi Uhuru Wasichana, Farida Kisenga, aliishukuru DART kwa kuamua kuanzisha utaratibu huo ambao unawawezesha wanafunzi kwenda na kurudi shule bila usumbufu.

Alisema utaratibu huo umekuja wakati mwafaka shule zimefunguliwa na idadi ya wanafunzi imeongezeka maradufu kuhitajika usafiri wa kutosha kuwafikisha shule na mkiwarejesha nyumbani nyakati za jioni.

"Huu ni utaratibu mzuri sana kwa kweli DART wanastahili pongezi kwasababu wanapunguzia watoto wetu matatizo, lakini usimamiwe vizuri, ili uwe endelevu isiwe mwanzoni tu hapa halafu watoto wakarudi kule kule kusukumana na watu wa daladala," alisema mzazi huyo.



Baadhi ya wanafunzi wakijisomea kwenye basi la mwendokasi, lililokuwa likitoka Kimara kwenda Kivukoni jijini Dar es Salaam jana, baada ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), kutenga mabasi maalumu ya kubeba wanafunzi pekee nyakati za asubuhi na jioni, ili kuwarahisishia usafiri wa kwenda shule na kurudi nyumbani. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Samia: Dhamira ni kuwa na darasa moja wanafunzi 45

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Muungano, zimedhamiria kufikia lengo la darasa moja kuwa na wanafunzi 45.

Pia amesema serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ustawi wa jamii ikiwamo elimu, maji na afya ili wananchi waweze kunufaika na huduma hizo.

Rais Samia aliyasema hayo jana, wakati akifungua Shule ya Msingi ya Mwanakwerekwe, ikiwa ni maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus.

Rais Samia alisema serikali itaendelea kuhakikisha wananchi wote wanapata haki ya elimu kwa kuimarisha miundombinu ya shule inayoendana na ongezeko la idadi ya watoto wanaohitaji kupatiwa elimu bora.

"Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na ya Muungano, zitahakikisha kunakuwapo mazingira bora ya kujifunza na kufundishia, kwa kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani, ili kufikia lengo la wanafunzi 45 kwa darasa," alisema Rais Samia.

Kadhalika, Rais Samia alipongeza Wizara ya Elimu Zanzibar, kwa kuunda kikosi kazi cha kuishauri serikali kufikia mageuzi muhimu ya elimu, kukidhi mahitaji ya dunia ya sayansi na teknolojia karne ya 21.

"Utekelezaji wa Dira ya Zanzibar ya 2050 pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Taifa, unategemea upatikanaji wa wataalamu kupitia sekta ya elimu. Serikali haina budi kuimarisha wataalamu kwa kuwapatia fani zinazoendana na mahitaji.

"Kuiwezesha Zanzibar kufaidika na matumizi ya rasilimali ya bahari kupitia mkakati wa kuimarisha Uchumi wa Buluu."

# Mahakama yaelezwa mwanamke alivyotumikishwa kingono Iraq

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa mashtaka umeieleza Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jinsi mwanamke wa kitanzania alivyosafirishwa kwenda nchini Iraq, kutumikishwa kazi za ndani na kufanyishwa ngono za watu wengi.

Imedaiwa mwanamke huyo aliona tangazo la kazi kwenye mtandao wa kijamii nchini Uturuki, lakini alipofika Dubai alihamishiwa kwenye ndege nyingine na kupelekwa Iraq kutumikishwa.

Wakili wa Serikali, Mosie Kaima, alidai hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ramadhani Rugemarila wakati akimsomea maelezo ya awali mshatakiwa Mohamed Salehe, kuhusu shtaka la kusafirisha binadamu.



Kaima alidai kuwa Juni 11, 2021 mlalamikaji Rahma Yusuph, alikutana na wanawake wawili na mshtakiwa eneo la Kipawa kwa ajili ya kuchukua hati zao za kusafiria na kusaini mikataba ya kazi.

Hata hivyo, mshtakiwa Salehe hakuwapatia mikataba ya kazi badala yake aliwapa hati zao na kumuita dereva teksi na kumtaka awapeleke wanawake hao Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

Alidai, walipofika uwanjani hapo, walipokewa na mtu mwingine aliyewapa maelezo kuwa watapanda ndege ya Shirika la Ndege Fly Dubai huku Rahma akiamini kuwa wanakwenda nchini Uturuki.

Alidai walipofika Dubai walishangaa kuhamishiwa kwenye ndege nyingine iliyokuwa inakwenda nchini Iraq eneo la Kurdistan na walipofika walichukuliwa na ofisa ambaye hawamfahamu na kuwaweka kwenye chumba kimoja cha ofisi.

Kadhalika, aliendelea kudai walifungiwa kwenye chumba hicho na kuporwa hati zao na walikuwa wakipewa mlo mmoja kwa siku wakiwa ndani ya chumba hicho na wanaume wenye asili ya kiarabu walikuwa wakienda kuwachukua huku yeye akichukuliwa mara tatu kwenda kufanyishwa kazi.

Rahma alidai kuwa, alipoona mateso yanazidi aliwasiliana na mshtakiwa na kumueleza amfanyie mpango arudi Tanzania kwa sababu anapigwa sana, anapewa mlo mmoja kwa siku, akiumwa hatibiwi na hapumziki.

Pia, alidai alikuwa akilazimishwa kumsafisha paka na kumbembeleza bila kupewa mshahara na kufanyishwa ngono kwa nguvu kwenye makundi.

Hata hivyo, alidai kuwa mshtakiwa alimwambia alipe kwanza fidia ya Dola za Marekani 4,000 kwa sababu yeye ndiye amekatisha mkataba.

Kutokana na hali hiyo, Rahma alidai kuwa aliwatafuta ndugu zake ambao walienda kutoa taarifa polisi na mshtakiwa alikamatwa na kukiri kuhusika na kumsafirisha mlalamikaji kwenda Iraq.

Imedaiwa kuwa mshtakiwa alimrudisha nchini Rahma kwa gharama zake, na Agosti 19, 2022, alitoa maelezo yake polisi kuhusu kilichotokea hadi yeye kufika Iraq.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Januari 25, 2023 kwa ajili ya kutajwa.

Jana kesi ilishindwa kusikilizwa kutokana na Kaima kudai mshtakiwa ameandika barua ya kuingia makubaliano ya kumaliza kesi hiyo na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP).

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
12.01.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumatatu tarehe 16-01-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kilombero** kupitia Mikumi, gari hiyo ina namba za usajili:
**T 631 DFA / T 837 DJB T 188 DFC / T 887 DJB**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 26.00**
**Upana - mita 5.10**
**Kimo - mita 4.70**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero** kupitia Mikumi, gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

217225002

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
12.01.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumatatu tarehe 16-01-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero** kupitia Mikumi, gari hiyo ina namba za usajili: **T 973 DTN / T 568 EAZ**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 20.00**
**Upana - mita 4.70**
**Kimo - mita 5.60**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero** kupitia Mikumi, gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

# Mchakato mapitio ya sera, mitaala mipya wakamilika

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, amesema serikali imekamilisha mchakato wa mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na mitaala mipya ya elimu.

Amesema kinachosubiriwa ni mchakato wa ndani ya serikali, kabla ya kuandaa kongamano maalumu la kitaifa la kukusanya maoni ya wananchi.

Prof. Mkenda alizungumza hayo juzi na wakuu wa vyuo vya ualimu Kanda ya Kaskazini, maofisa elimu, wakufunzi na wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Marangu wilayani Moshi, mkoani Kilimanjaro, kuwa kinachosubiriwa ni mchakato wa ndani ya serikali.

Mapitio hayo yanaihusisha pia Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978, ili kuifanya sekta hiyo kuendana na mabadiliko ya elimu duniani.

"Mnaweza kufikiria Marangu ianze kutoa digrii katika lugha na itatusaidia sisi kupata wakalimani wengi duniani, yaani mtu akija kuchukua digrii yake achukue digrii ya lugha, yaani ajue Kiswahili vizuri, Kiingereza kizuri, Kiarabu na Kifaransa kizuri, na pengine sisi huko duniani tupeleke wakalimani."

Katika mapitio hayo ya sera na mitaala, Waziri Mkenda, alisema serikali imezingatia ujenzi, mapitio na maboresho ya vyuo vyote vya ualimu, kwa kuwa ni mboni au jicho la elimu nchini.

Alisema kwa sasa kuna jumla ya vyuo 35 vya serikali na vyuo vingine vya taasisi na vya binafsi na kwamba kuna kila sababu ya kuvitazama kwa umakini mkubwa ili kuboresha sekta ya elimu nchini.

Alikiagiza Chuo cha Ualimu cha Marangu, kufufua maabara za lugha ikiwamo Kiingereza na Kiswahili, kama hatua mojawapo ya kurejesha hadhi ya mitaala iliyokuwa ikichochea maendeleo ya elimu nchini.

Vilevile, amevitaka vyuo vyote vya ualimu nchini, hususani vinavyofundisha lugha, kujiandaa kufundisha lugha nyingine za kimataifa zinazochipukia ulimwenguni ikiwamo Kifaransa, Kichina, Kihispania na Kiarabu.

Kadhalika, serikali itaendelea kuvipa msukumo vyuo vya namna hiyo nchini kwa kuwa vinatoa wabobezi wa lugha na pengine wengeweza kwenda kuwa wakalimani wazuri kwa mataifa mengine na nchi kwa ujumla.

"Chuo hiki tukipe msukumo maalumu kwenye lugha kwa sababu ndiko mlikoanza, nafikiri mlikuwa na maabara ya Kiingereza tuifufue, ya Kiswahili iko wapi, tuzifufue hizi maabara zetu ili tuendelee kutoa walimu wabobezi zaidi kupitia chuo hiki," alisisitiza.

**KIINGEREZA**

Kuhusu mpango wa kuimarisha taaluma katika Mkoa wa Mara, baada ya kuwekwa zuio kwa wanafunzi kuendelea na masomo hadi wamalize wiki nane za kujifunza Kiingereza, Waziri Prof. Mkenda, alisema tayari amezungumza na Mkuu wa mkoa huo, Meja Jenerali Suleiman Mzee na kumshauri wasitishe na kutafuta ubunifu mwingine.

"Kuna mkoa mmoja, ofisa wake, amesema wanafunzi wetu wakimaliza darasa la saba na wakiingia sekondari, inabidi kwanza wakae wajifunze lugha kabla hawajaanza masomo. Nimeongea na Mkuu wa Mkoa wa Mara, nimemshauri nimemwambia tusisitishe tutafute ubunifu mwingine, lakini mwarobaini wake utakuja kupitia mapitio ya sera na mitaala mipya.

"Lakini tunaelewa kabisa changamoto iliyoko hiyo ya kuwafundisha watoto, darasa la nne, la sita na la saba. Unafundisha Kiingereza, unamaliza hawezi kuongea Kiingereza. Hiyo si dalili tu kwamba hatufundishi vizuri, Kiingereza tuna kazi kubwa ya ku-improve (kuboresha) kufundisha.

Kauli ya waziri inatokana na taarifa iliyotolewa na ofisa mmoja wa Mkoa wa Mara, aliyenukuliwa akisema, "Katika kuimarisha taaluma, tumetoa maelekezo kwamba Mkoa wa Mara, kuanzia Januari 9, wanafunzi wote ambao wataanza kidato cha kwanza, wataanza na 'English Orientation' (uelewa wa lugha ya Kiingereza) kwa kipindi cha wiki nane.

"Na tutawa-'test' wanafunzi wale (tutawapima), hakuna kusoma masomo ya kawaida, watafanya 'English Orientation', baada ya wiki nane tuta-watest wanafunzi, tutajua viwango vyao vya uelewa wa Kiingereza.

"Na la tatu katika hilo, tumepiga marufuku lugha ya Kiswahili kutumika kwenye shule zetu zote za sekondari.

"Tunahitaji tuhakikishe kuwa wanafunzi wanamudu lugha ya Kiingereza kama ambavyo Sera ya Elimu na Sheria ya Elimu inavyoelekeza. Tumebaini kuwa lugha ile inasababisha wanafunzi wengi wanafeli kwa sababu hawamudu kujieleza."

SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

WAKALA WA CHAKULA DAWA NA VIPODOZI

# MAFANIKIO YA WAKALA WA CHAKULA DAWA NA VIPODOZI NA MIAKA 59 YA MAPINDUZI

Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Afya iliyoanzishwa chini ya kifungu 3 (1) sheria nambari 2:2006 na marekebisho yake Sheria nambari 3:2017 ya Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi.

Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi katika kuleta ufanisi wa kazi zake za kila siku ina idara zifuatazo:-
Idara ya Huduma za Wakala,
Idara ya Udhibiti Usalama wa Chakula,
Idara ya Dawa na Vipodozi
Idara ya Huduma za Maabara.

Jukumu la Wakala wa Chakula na Dawa (ZFDA) ni kulinda na kuimarisha Afya za Wananchi wa Zanzibar kuhakiksha Ubora na Usalama wa Chakula, Dawa, Vipodozi, Vifaa Tiba na Vitendanishi. Jukumu hili linafikiwa kwa kuhakikisha Bidhaa zinazotarajiwa kuingia na zinazozalishwa nchini zinakaguliwa na pia zinachunguzwa na Maabara ya ZFDA kabla ya kuruhusiwa kuingia kwenye soko la Zanzibar.

Aidha, ZFDA inafanya kazi ya Ukaguzi na Usajili wa majengo na sehemu zote ambazo zinashughulika na Uzalishaji, Uhifadhi, Usambazaji, Uuzwaji na Ufungashaji wa Bidhaa ambazo ZFDA inazisimamia. Mfano wa Majengo ambayo ZFDA inayakagua na kuyasimamia ni Viwanda, Migahawa, Bekari, Machinjio, Mabucha, Vioski, Maduka ya Chakula, Maduka ya Dawa za Binadamu na Mifugo, Maduka ya Vifaa Tiba, Gari za Kusafirishia Chakula, Mashine za kusagia nafaka na Maduka ya Vipodozi.

Wakala wa Chakula na Dawa imepata mafanikio mbali mbali ya utekelezaji wa mipango na miradi ya Serikali ndani yam waka mmoja katika katika Serikali a Mapndzi a Zanzibar kutimia miaka 59 ya mapinduzi Zanzibar hivyo kupitia mafanikio hayo na utekelezaji wa kazi za ZFDA inahakikisha Bidhaa zote zinazozalishwa na zinazoingia nchini zinakua Bora na Salama kwa Afya za wananchi.
Mafanikio hayo ni kama yafuatayo:-

**Kumalizika kwa jengo jipya la Maabara ya kisasa ya ZFDA**
Mafanikio makubwa ambayo ZFDA imeyapata katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kumalizika kwa Jengo jipya la maabara ya kisasa ya ZFDA, ambapo Fedha zilizotumika katika mradi huo ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asili mia 100%. Aidha Maabara hiyo inawataalamu wabobezi katika ufanyaji kazi na itafanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu ili kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Jengo hilo lina maabara tatu ambazo ni Maabara ya Usalama wa chakula, Maabara ya Dawa na Vipodozi na Maabara ya Vimelea (Microbiology) Hivyo ZFDA Daima itajivunia mafanikio ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutimia miaka59 ya mapinduzi kwa kuhakikisha Bidhaa za Chakula, Dawa, Vipodozi na vifaa vya Utabibu vinakuwa Bora na Salama kwa matumizi ya wananchi.

**Kupata Ruzuku kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.**
Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe, Dr Hussein Ali Mwinyi inaendelea kupata ruzuku kama ilivyokuwa kwa awamu nyengine, Hivyo basi hii inaonesha ruzuku imeengezeka kwa kiwango kikubwa ili ZFDA iweze kujiwezesha na kufanya kazi zake kwa kuangalia mpango mkakati na kuhakikisha majukumu ambayo imejiwekea inayatekeleze kwa vitendo ili kudhibiti Ubora, Ufanisi na Usalama wa Chakula, Dawa, Vipodozi na Vifaa vya utabibu.

**Ununuzi wa vifaa vya Maabara.**
Wakala wa Chakula na Dawa imepata vifaa vipya na vya kisasa vya kimaabara kwa ruzuku ya Serikali na kupitia wahisani wa kimaendeleo kama vile Global Fund (GF), Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination (TANIPAC) n.k ili kufanya kazi zake kwa weledi kwa ajili ya kuchunguza Bidhaa mbali mbali zinazo ingia nchini ili kuhakikisha jamii inapata afya bora na salama.

**Vifaa hivyo ni kama vifuatavyo:-**

- HPLC-(high performance liquid chromatograph) ni kifaa kinachotumika kuchanganua, kutambua na kupima kiwango na aina ya sumukuvu, kifaa hichi kimetolewa na (TANIPAC).
- GLOBAL FUND – Gas Chromatograph Mass Spectmatry (GCMS) – Kifaa kinachotumika kwa uchunguzi wa dawa.
- Vicam-inapima sumu kuvu (unyevu nyevu)
- Incubator-kuotesha vijidudu kwaajili ya kufanya uchunguzi wa maikrobaiolojia (microbiology)
- Autoclave-inatumika kwa ajiili kuua vijidudu
- Drier box (Olive) ni kupima unyevu unyevu katika sampuli.
- Bio safety- ni kifaa kinachotumika kuzuia vijidudu visisambae ndani ya chumba cha maabara wakati wa kufanya uchunguzi.
- Fum-hood – Ni kifaa kinachotumika kuzuwia kemikali isisambae ndani ya chumba cha maabara wakati wa kufanya uchunguzi.
- Gas Chromatography (GC) ni kifaa kinaachotumia gesi tukufu kuchanganua, kutambua na kupima kiwango cha aina ya kemikali iliyomo katika mchanganyiko.
- Cenrifuge- Ni kkifaa kinachotumika kutayarisha sampuli kabla ya kuziingiza katika mashine Kwa ajili ya uchunguzi.

**Kutumika kwa mfumo wa kielektroniki wa (ZFDA Ims web portal)**
Mfumo huu umerahisisha utendaji wa kazi za Wakala wa Chakula na Dawa kwa kuwarahisishia kwa wafanya biashara kwa kuomba vibali sehemu yoyote na muda wowote (masaa 24) ili kurahisisha kazi za ZFDA. Na kwa upande wa wafanya biashara umewarahisishia biashara zao kwa kutoa mizigo kwa muda mfupi na kuomba kibali na kupatiwa kwa muda mfupi na kumfanya mfanya biashara kupata bidhaa zake kwa wakati ili kupunguza msongamano bandarini na vile vile mfumo huu umeleta mafanikio makubwa kwa Taasisi pamoj na kufata huduma Ofisini kwa wafanya biashara ili kuleta maendeleo ya Zanzibar kwa ujumla.

**Kupata ithibati ya kimataifa (ISO 9001:2015 Certification)**
Pia inategemea kupata Ithibati ya kimataifa ya Utoaji Huduma Bora za Maabara (Accreditation) ISO 17025:2017 ya ZFDA ili kuzidi kutambulika kitaifa na kimataifa katika utekelezaji wa majukumu yake.

**Mashirikiano ya kikanda na kimataifa**
Kazi za Wakala wa Chakula na Dawa zimeboreka zaidi kwa kufanya kazi kwa kushirikiana na programu za Kikanda na za Kimataifa, ZFDA kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki inaendelea kufanya mashirikiano na Jumuiya katika kufanikisha kazi zake kwa kupitia mradi wa uwiano wa Dawa (East Africa Medicines Regulatory Harmonization Programe), kwa sasa Wakala inashiriki katika programu za pamoja za kikanda (Joint EAC Activities) ambapo mradi huu unawashirikisha wataalamu wa kikanda katika Nyanja ya kutathmini na kusajili dawa kwa pamoja katika nchi zote wanachama wa jumuiya pamoja na kukagua viwanda vinavyozalisha dawa.

**Kuengezeka kwa Uelewa kwa wananchi.**
ZFDA imepata mafanikio makubwa kutokana na uelewa kwa wananchi kuelewa juu ya usalama wa Chakula Dawa na Vipodozi umeengezeka kwa kwa kiasi kikubwa kwa jamii , Elimu hiyo inatolewa kupitia mambo mbali mbali kama-:

- Kufanya vipindi vya Radio na kutoa matangazo.
- Kutoa Makala.
- Kushiriki maonyesho mbali mbali.
- Kufanya kaz kwa kufuata mkataba wa huduma kwa wateja.


**Kupungua kwa bidhaa duni zisizofaa kwa matumizi ya binaadamu.**
Kwa kiasi kikubwa Bidhaa zisizofaa kwa matumizi ya binaadamu zimepungua kutokana na uwajibikaji kwa wafanya biashara pamoja na wananchi kwa ujumla. Tathmini inaonyesha jumla ya Bidhaa zilizoteketezwa ni ishirini na tisa elfu na tatu (29,003), Tathmini ya bidhaa zilizorejeshwa nje ya nchi ni Sabiini na nane elfu, mia nne hamsini na nane (78,458). Jumla ya bidhaa zote zisizokidhi vigezo kwa mwaka 2021 hadi mwaka 2022 ni 107,500. ZFDA inafanya ukaguzi sehemu mbali mbali za bandari ili kuhakikisha bidhaa zote zinazoingia nchini zinachunguzwa katika Maabara zetu ili kupunguza Didhaa duni zisizofaa kwa matumizi ya binaadamu.

Hivyo basi kutokana na Mafanikio iliyoyapata Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi(ZFDA) kufikia miaka 59 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar katika uongozi wa Mh. Dk. Hussein Ali Mwinyi mafanikio haya yataifanya ZFDAkufanya kazi zake kwa uweledi na kuhakikisha inadhibiti Ubora na Usalama wa Chakula, Dawa vipdozi, na vifaa vya Utabibu.

“Kwa pamoja tunalinda afya ya jamii”
**www.zfda.go.tz /Email: info@zfda.go.tz**

# MAADHIMISHO YA MIAKA 59 YA MAPINDUZI MATUKUFU YA ZANZIBAR

59 MIAKA YA MAPINDUZI



Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi

Ofisi ya Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi, Menejimenti na Watanzania wote inaungana na Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Raisi wa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika kuadhimisha miaka 59 ya mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya 1964.

**“MAPINDUZI DAIMA”**

**OFISI YA UNGUJA**
Tomondo ROad, Mombasa Area,
P.o.box 3595, Zanzibar,
Tel +255242233959,
Fax 255 242233959,
Website www.zfda.go.tz,
Email info@zfda.go.tz

**OFISI YA PEMBA**
Kilimandege,Wete Pemba
TEL; 255242454050
Website www.zfda.go.tz
Email; info@ zfda.go.tz



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

T7226302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo kuwapo matroni kwenye mabasi ya shule litekelezwe

**BAADA** ya kutokea kwa matukio ya unyanyasaji unaodaiwa kufanywa na makonda na madereva kwa wanafunzi wanaosoma shule zinazotoa usafiri wa mabasi, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, alitoa agizo la wamiliki wa shule hizo kuweka matroni atakayewasimamia.

Matukio yaliyoripotiwa ni madai ya makonda na madereva kufanyia ukatili wa kingono baadhi ya wanafunzi wanapowarudisha nyumbani nyakati za jioni.

Kibaya zaidi, inadaiwa makonda hao na madereva hufanya vitendo hivyo kwa kumchangia mtoto mmoja.

Ni matumaini yetu kuwa agizo hilo litatekelezwa na wamiliki wa shule zinazotoa huduma ya usafiri kwa wanafunzi hao ili kuwaepusha na unyanyasaji huo wanaofanyiwa huku wakitishwa watawaua kama watasema kwa wazazi wao.

Jukumu la kuwaangalia watoto ni la jamii na inapotokea wanafanyiwa vitendo vibaya ni lazima hatua zichukuliwe kwa kuadhibiwa waliohusika kufanya hivyo.

Jana wakati Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, akitembelea shule kuangalia wanafunzi walioripoti, aliagiza shule binafsi zote kuweka mwangalizi wa kike (matron) katika kila gari la wanafunzi ili kuepusha wanafunzi kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji au ukatili wa kijinsia.

Alisema katika wilaya yake ya Kinondoni, shule zote za binafsi zenye mabasi wameweka matron na hayo ni maamuzi ya serikali ya wilaya na lengo ni kutengeneza mazingira mazuri kwa watoto kutopata athari za mashambulizi au unyanyasaji wa kijinsia.

Mkuu huyo alisema asingependa katika wilaya yake yaliyotokea mwaka jana yatokee mwaka huu na kwamba ameshaunda timu ikijumuisha madawati ya jinsia kutoka Jeshi la Polisi na Maofisa Ustawi wa Maendeleo ya Jamii kwa pamoja kupita shule zote kuhakikisha mabasi yote ya watoto yana matron kule ndani.

"Lengo letu tunataka kila mzazi anapokabidhi mtoto anajua yuko maeneo salama, tunataka maeneo ya shule zetu za watoto mpaka mabasi yanaendelea kuwa salama kwa watoto wetu. Hatutavumilia shule yoyote ambayo kwenye basi itaweka msaidizi wa kiume, tunataka kuepukana na mazingira hatarishi kwa watoto wetu."

Hatua hiyo ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni ni ya kupongeza ili kuwanusuru watoto wasiendelee kufanyiwa ukatili na kuchukia shule.

Wakuu wengine wa wilaya wanatakiwa kuvalia njuga suala hilo ili kukomesha kabisa matukio hayo yanayokwenda kinyume na maadili.

Katika kuonesha kuwatia moyo watoto waliofaulu kuingia kidato cha kwanza katika wilaya yake pamoja na walimu wao, Gondwe aliagiza wanafunzi wote waliofaulu kwenda sekondari kwenye wilaya yake ambao hawana sare, kuripoti shuleni na kuanza masomo kwa kuvaa sare walizotoka nazo shule ya msingi.

Alisema ni vyema wanafunzi hao wakatumia sare walizokuwa wakitumia shule za msingi kuliko kukosa masomo.

"Wazazi wote ambao watoto wao wanaingia kidato cha kwanza wasijali, hata kama watoto wao hawana sare za shule, wahakikishe wanaenda shuleni, hatutaangalia kwamba hana sare au nini. Hatuwezi kusubiri mtoto akose masomo, hata kama ana sare zake alizozitumia shule ya msingi aje tu hivyo hivyo na mambo yatakwenda taratibu akiendelea kutumia hizo sare za msingi," alisema Gondwe.

"Haitakuwa jambo jema watoto wamefaulu halafu wanabaki nyumbani kwa sababu eti hawana sare za shule, hatutaki kuona mtoto yeyote anabaki nyumbani kwa sababu hiyo wakati analipiwa ada na Rais Samia Suluhu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Tatizo la wanafunzi kuandika matusi kwenye mitihani likiachwa kuendelea, shida inakuja

**ELIMU** ni nini? Inatajwa kuwa mbinu, maarifa na uelewa unaomfanya anayejifunza kubadilika, akimudu vyema mahitaji ya kukidhi yake ya msingi kimaisha, mahali aliko au kunakomuhusu.

Pia mtu anapoipata elimu hiyo ambayo ina mwongozo wa mtaala pale inapokuwa rasmi, anaangukia katika manufaa kwamba atayamudu mazingira na vyote vinavyopatikana mahali hapo, ikiwamo mazingira, mimea, viumbe na binadamu wenzake mahali hapo.

Ili kuwa na namna inayojidhihirisha katika hilo, huwa wahusika wanaojifunza kufanyia tathmini, katika mazingira rasmi hukutana na mtihani au majaribio unaowapima uelewa wa walichojifunza.

Mara zote huo mtihani huwa ni kigezo cha ama kuvusha au kusubirisha, hata pia kumuengua kwa hatua zaidi. Si jambo rahisi, ila ukweli unabaki palepale kwamba una umuhimu mkubwa kwa wote.

Hata hivyo, mara nyingi wanajamii tumekuwa tukiona baadhi ya wafanyaji mtihani shuleni, wanaibuka na matendo tata kama vile kuandika lugha chafu katika karatasi zao za mitihani ya mwisho ya taifa.

Mbali ya hali hiyo, wafanyaji mtihani wengine huangukia kuchora yasiyohusiana na maswali yao, hata haifanani na dhumuni la mtihani kwa ujumla. Watu kwenye karatasi za mtihani, wanathubutu hata kuiangukia kuandika nyimbo, badala ya kujaza kile wanachopaswa kuandika katika karatasi la mtihani, kujibu maswali anayoulizwa. Hapana shaka ni walakini mkubwa kwa watahiniwa, tena katika umri mdogo walio nao.

Inawezekana kabisa sababu kuu hata kugeukia kuwa chanzo cha hilo la tabia chafu, ni kutokuwapo sheria zinazowabana wafanyaji mtihani hao. Ukweli katika mtazamo wangu, naona kuachwa huko kunajenga tabia ya matendo haya kujirudia katika mazingira hayo ya tabia sugu.

Kila mwaka na hasa kunapokuwapo mitihani ya mwisho ya mwaka, baadhi ya wahitimu badala ya kujibu maswali walioulizwa, wao wanajibu vitu visivyohusiana kabisa na maswali waliotakiwa kuyajibu.

Ni hali inayotoa picha ya dhihaka na dharau hata kwa walimu wao ambao wametumia nguvu kubwa kufikia kuwaezesha vijana hao kufanya mtihani.

Katika kutoa hoja ya kukomeshwa vitendo hivyo, Mjumbe wa Kamati kutoka Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Nelson Mabula, anashauri kunatakiwa wanafunzi ambao watabainika kuandika maneno yasiyofaa katika mitihani yao na wachukuliwe hatua.

Anafafanua kuwa mbali na kuchukua hatua, wanafunzi wakorofi watajwe majina yao na shule walizosoma na kupofanyika hivyo, inawezekana kukusaidia kukomesha matukio yaliyo sasa katika hali endelevu.

"Tunasikia tu katika mitihani, baadhi ya wanafunzi wamejaza lugha mbaya, huku wengine wakichora katuni. Sasa taarifa zinatolewa, lakini hawatajwi wala kutajwa shule zao, kwa kufanya hivyo kunachangia matukio kuendelea kutokea," anasema.

Mabula anaongeza kuwa, kama wanaotukana au kuchora katuni katika mitihani yao hawachukuliwi hatua, ni wazi matukio hayo yataendelea kutokea kila mwaka.

Anataja changamoto nyingine inaanzia kwa baadhi ya wazazi hawawajibiki kuwalea watoto vizuri na kuliacha hilo kubaki kuwa jukumu la walimu shuleni.Mjumbe huyo wa CWT na mwalimu kitaaluma, anarejea takwimu zake kwamba,

asilimia 80 ya wazazi hawawajibiki na watoto wao, ilhali kinyume chaka wazazi wanatakiwa watenge muda kwa ajili ya kufahamu maendeleo ya watoto wao.

Anaongeza kuwa pale mzazi asipotenga muda wa kumfuatilia mtoto, ajue yuko katika hatua za kumpoteza. Hivyo, anasisistiza kwamba jukumu la mzazi ni kuhakikisha anamfuatilia mtoto wake kwa kina na kamwe isibaki kuwa kazi ya kumwachia mzazi mwalimu peke yake.

Hapo anaunganisha na wito wake binafsi, kuwataka walimu wenzake waendelee kufanya kazi kwa kujituma, ili kuwawezesha wanafunzi kusoma na kuandika kwa ufanisi.

Anasema zaidi kuwa walimu watengeneze mazingira wezeshi ya kuwasaidia watoto kuelewa masomo, kwa wale wanaosuasua katika kumudu taaluma darasani.

Pia anaiomba serikali ifanye utaratibu wa kuwataja watoto waandikaji mambo yasiyofaa katika mitihani yao ya mwisho, huku wakibanwa wataje wenzao.

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# OFISI YA RAISI KATIBA SHERIA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA.

Suala la kuwapatia wananchi taarifa ni haki ya msingi kama ilivyobainishwa katika Katiba ya Zanzibar ya 1984 katika Ibara ya 18 (2), ninanukuu:

**"Kila raia anayo haki ya kupewa tarifa wakati wowote kuhusu matukio mbali mbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii."**
Mwisho wa kunukuu.

Kwa hivyo, nikiwa Waziri ninayesimamia masuala ya sheria, napenda niwe mstari wa mbele kulitekeleza jambo hilo, hasa katika kipindi kama hiki ambapo tunafanya Maadhimisho ya Sherehe za Mapinduzi na pia tumekamilisha miaka miwili tangu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Nane ilipoingia madarakani.

Tunaendelea kushuhudia mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo tangu Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi ilipoingia madarakani. Mafanikio hayo yanaonekana katika Sekta zote kiuchumi na kijamii. Tumepiga hatua katika Utekelezaji wa ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni za Uchaguzi. Vile vile, tumepata mafanikio makubwa katika Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025, kama ilivyoelezwa siku chake zilizopita katika vikao vilivyofanyika Dodoma.

Mafanikio tunayoendelea kuyapata pia ni sehemu ya utekele`zaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 pamoja na Mipango Mikuu ya Maendeleo iliyopangwa na Jumuiya za Kimataifa kwa upande wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla.

Kwa hivyo, kabla ya kuanza kuelezea mipango iliyotekelezwa na Wizara yetu hii, nachukua fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kushika wadhifa wa Makamo Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, hatua ambayo itampa nafasi kubwa zaidi ya kusimamia Ilani na yale yote aliyodhamiria kuyafanya kwa maendeleo yetu. Kuchaguliwa kwakwe kwa zaidi ya aslimia 99 ya kura zilizopigwa ni kielelezo thabiti cha imani ya Wana CCM na wananchi tuliyonayo kwake kutokana na uongozi wake thabiti.

Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kuendelea kuiongoza Zanzibar vizuri na juhudi zake katika kudumisha umoja, mshikamano, amani pamoja na utulivu.

Kwa upande wa Sekta ya Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora, tumepata mafanikio makubwa. Kwa kuwa mambo tuliyoyatekeleza na mafanikio tuliyopata ni mengi na muda ni mchache, naomba mniruhusu niyaeleze baadhi tu ya mambo na mafanikio hayo.

Kwa upande wa MAHAKAMA, Serikali imefanya juhudi kubwa katika kuhakikisha kwamba, Muhimili huu unaendelea kutekeleza majumu yake ukiwa huru na kwa ufanisi, kwa lengo la kuharakisha uendeshaji wa kesi, Serikali imeongeza idadi ya Majaji, Mahakimu na Makadhi. Kwa mfano, Idadi ya Majaji imeongezeka kutoka wanane (8) mwaka 2021, hadi 11 mwaka 2022, wakiwemo Majaji wanne (4) wanawake.

Vile vile, Mahakama kwa kushirikiana na wahusika wa Haki Jinai imeanzisha utaratibu wa kuendesha vikao maalum chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Jaji Mkuu, kwa lengo la kuharakisha usikilizaji wa mashauri yanayowasilishwa Mahakamani.

Aidha, Mahakama maalum ya kusikiliza kesi za udhalilishaji imefunguliwa rasmi kama ilivyoagizwa na Mheshimiwa Rais. Hatua hiyo ya kimkakati ina lengo la kuongeza kasi katika mapambano dhidi ya vitendo vya udhalilishaji ambavyo vinaonekana kuwa vimekithiri katika Nchi yetu.

Vile vile, Serikali imefanya juhudi maalum za kuimarisha mfumo wa Haki Jinai sambamba na kuiwezesha OFISI YA MKURUGENZI WA MASHATAKA kuongeza kasi ya upelelezi wa kesi zinazoripotiwa na kusajiliwa. Katika kipindi cha Octoba, 2020 hadi Oktoba, 2022 jumla ya kesi 971 za makosa mbali mbali zimeendeshwa katika mahakama za Unguja na Pemba.

Wizara yangu, kupitia TUME YA KUREKEBISHA SHERIA na kwa kushirikiana na Muhimili wa Kutunga Sheria, imefanya juhudi kubwa katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais linalotutaka tuwe na mkakati maalum wa kufanya marekebisho ya sheria ili kuondokana na sheria za zamani ambazo ni kikwazo kwa maendeleo yetu pamoja na zile zilizopitwa na wakati. Miongoni mwa kazi hizo ni Mapitio ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2 ya Mwaka 2011, Sheria ya Mufti, Nambari 9 ya Mwaka 2009, Sheria ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Sheria ya Jumuiya Nambari 6 ya Mwaka 1995 (The Societies Act).

Katika kipindi hiki cha miaka miwili, Serikali imefanya juhudi kubwa katika kuimarisha utendaji wa AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Jumla ya rasimu za Mikataba 390 inayohusu masuala mbali mbali zimefanyiwa mapitio na kutolewa ushauri. Aidha, juhudi kubwa zimefanywa katika kutoa elimu inayohusu masuala ya sheria kwa watendaji wa taasisi mbali mbali za Serikali.

Ndani ya kipindi hiki, Serikali ilipanga na kutekeleza mikakati maalum ya kuwapatia wananchi MISAADA YA KISHERIA ili kuimarisha upatikanaji wa haki na usawa kwa wananchi wote. Jumla ya Wananchi 2,395 wamepatiwa elimu ya kisheria. Aidha, tumezifuatilia kwa karibu taasisi zote zinatoa misaada ya huduma za msaada wa kisheria. Jumla ya watoa huduma za msaada wa kisheria 214 wamesajiliwa Unguja na Pemba.

Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora katika kipindi hiki cha miaka miwli, imefanya kazi kubwa ya kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais na maelekezo ya Ilani ya CCM kuhusu uimarishaji wa maslahi ya wafanyakazi.

Tumekamalisha na kuweka sawa MIFUMO na MIUNDO ya UTUMISHI, ambapo hivi sasa ulipaji na upokeaji wa mishahara na maslahi mengine ya kila mtumishi vinazingatia pamoja na mambo mengine vikiemo kiwango cha elimu, uzoefu, ari ya utendaji, muda wa utumishi pamoja na utaalamu katika kada husika.

Hatua hiyo, vile vile, imetuwezesha kwa kiasi kikubwa kuondoa malalamiko yaliyokuwepo awali, hasa suala la kutokuwepo kwa mazingatio maalumu juu ya muda wa utumishi na uzoefu.
Kukamilika kwa miundo ya utumishi kumerahisisha utekelezaji wa agizo na ahadi ya kuongeza mishahara kwa Watumishi wa Umma. Viwango vya mishara vimepandishwa tangu mwezi Julai mwaka huu. sawa na ongezeko la asilimia 36

Wizara yangu, inaendelea kuzifanyia kazi changamoto na kasori ndogo ndogo zilizojitokeza katika utekelezaji wa agizo la kupandisha mishahara pamoja na uandaaji wa miundo na mifumo ya utumishi.

Jumla ya nafasi za ajira 2,559 zimetolewa katika wizara, mashrika ya umma na taasisi mbali mbali za Serikali ndani ya kipindi cha miaka miwili. Hivi sasa, nafasi nyengine za ajira zinaendelea kutangazwa kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo.

Juhudi kubwa zimefanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya nane katika kuimarisha OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ndani ya kipindi hiki cha miaka miwili. Hatua hiyo imeiwezesha taasisi hii kufanya kazi za Udhibiti na Ukaguzi katika Wizara na Taasisi za Serikali pamoja na miradi ya maendeleo kwa ufanisi na uwazi zaidi. Tunaendelea kushuhudia Mheshmiwa Rais akipokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hadharani na mbele ya vyombo vya habari. Uamuzi huo unafurahiwa na wananchi. Hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa kwa wale wahusika wanaohitaji kuchunguzwa zaidi baada ya ripoti hiyo kuwasilishwa.

Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa maelekezo na miongozo anayotupa katika kuimarisha utendaji wa MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI (ZAECA). Ndani ya kipindi hiki cha miaka miwili tumeshudia mafanikio makuwa yaliyopatikana na taasisi hii katika utekekelezaji wa majukumu yake. Jumla ya tuhuma au malamiko yanayohusiana na rushwa yamepokelewa na yamefanyiwa kazi.

Vile vile, katika kipindi hicho, ZAECA imeweza kuokoa na kurejesha mali Serikalini zenye thamani ya Shilingi 1,106,486,467. Aidha, ZAECA imetekeleza mikakati maalum ya kutoa elimu kwa jamii na taasisi za elimu kuhusiana na madhara ya rushwa ndani ya jamii na kwa maendeleo yetu.

Wizara yangu, kupitia TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA, imefanya kazi kubwa katika kuhakikisha kwamba viongozi wa umma wanatekeleza wajibu wao kwa kuzingatia sheria na maadili yanayoongoza kazi na dhamana walizopewa. Kila mwaka, Tume inaendesha kwa mafanikio zoezi la kujaza na kurejesha Fomu za Tamko la Mali na Madeni. Viongozi wanaobainika kukiuka maadili wanaripotiwa katika taasisi au mamalaka zao za uteuzi kwa ajili ya kuchukuliwa hatua stahiki.

WAKALA WA SERIKALI MTANDAO, imeunda na kuimarisha mifumo ya kisasa ya kielektroniki kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Serikali, utoaji wa huduma kwa wananchi pamoja na ukusanyaji wa mapato. Miongoni mwa mifumo iliyotengenezwa na kutolewa mafunzo ni pamoja na Mfumo wa ZanMalipo, Mfumo wa e-Office, Mfumo wa Bajeti na Matumizi ya Serikali (BAMAS) na Mfumo wa Manunuzi kwa Njia ya Mtandao (E- procurement). Aidha, taasisi hii, imeandaa miongozo 26 inayohusiana na usimamizi wa miradi, utaratibu wa matumzi ya taarifa, utengenezaji wa mifumo, matengenezo ya vifaa vya TEHAMA, usalama wa mfumo, utengenezaji wa nyaraka za TEHAMA, matumizi ya barua pepe na tovuti za Serikali.

Mambo mengine muhimu yaliyotekelezwa na Wizara yangu ndani ya kipindi hiki cha miaka miwili ni kuanzisha rasmi SKULI YA SHERIA ZANZIBAR. Skuli hii imeanzishwa kupitia Sheria Nambari 13 ya mwaka 2019 na imeanza kutoa mafunzo tarehe 17 Januari, mwaka huu, 2022 baada ya uteuzi wa Mkuu wa Skuli ya Sheria pamoja na Wajumbe wa Baraza la Skuli. Vile vile, tumepata mafanikio makubwa katika kukiimarisha CHUO CHA UTAWALA WA UMMA (IPA).

KAMISHENI WAKFU NA MALI YA AMANA pamja ya Ofisi ya Mufti imepata mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu yao. Kamisheni ya Wakfu imesimamia na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala muhimu yanayohusu mirathi, wakfu, Ibada ya Hijja, Zaka na ukusanyaji wa misaada na sadaka mbali mbai zinazotolewa na taasisi za ndani na nje ya nchi.

Aidha, kazi kubwa imefanywa na OFISI YA MUFTI katika Usajili wa Misikiti, Madrsa, Kuendesha mafunzo ya ndoa, kutoa fatwa katika mambo mbali mbali ya kiislamu, kusuluhisha migogoro ya ndoa na kutoa mafunzo ya ualimu kwa Waalimu wa Madrasa vile vile.

Aidha, Ofisi imeendelea kushirikiana na wafuasi wa dini nyengine kwa lengo la kuimarisha umoja, mshikamano pamoja na hali ya amani na utulivu hapa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla.

Ni dhahiri kwamba kila penye mafanikio hapakosi changamato. Miongoni mwa changamoto tunazoendelea kukabiliana nazo ni pamoja na uchakavu wa baadhi ya majengo ya ofisi zetu, ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi katika baadhi ya taasisi zetu, upungufu wa wataalamu na wenye ujuzi mahsusi na pia upungufu wa rasilimali fedha, hasa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Tunaendelea kupanga kutekeleza mipango mbali mbali kwa ajili ya kuzifanyia kazi changamoto hizi.

Mafanikio tuliyopata, vile vile, yamechangiwa na ushirikiano mkubwa uliopo baina ya Serikali ya Mapinduzi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa msingi huo, natumia fursa hii kutoa shukurani maalum kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa ushirikiano wake wa karibu na Rais wa Zanzibar pamoja na wananchi wote kwa jumla. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape afya njema na maisha marefu viongozi wetu hawa.

Baada ya kusema hayo, nawashukuru sana kwa kunisiliza

**Ahsanteni sana.**

# MAADHIMISHO MIAKA 59 YA MAPINDUZI MATUKUFU YA ZANZIBAR



59 MIAKA YA MAPINDUZI

OFISI YA RAISI, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA na Wawanzania wote inaungana na Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Raisi wa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika kuadhimisha miaka 59 ya mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya 1964.

**"MAPINDUZI DAIMA"**

**Ofisi ya Raisi Katiba Sheria utumishi na Utawala Bora**
**Simu 0773006789**
**Email: info@utumishismz.go.tz**
**MAZIZINI ZANZIBAR.**

Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

17225802

## SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

## WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

# MAFANIKIO YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI NA MIAKA 59 YA MAPINDUZI

Tunaendelea kushuhudia mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo tangu Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi ilipoingia madarakani. Mafanikio hayo yanaonekana katika Sekta zote kiuchumi na kijamii.

Katika mazungumzo na gazeti la nipashe ofisini kwake maisara DK. Abou Suleiman Jumbe, Katibu mkuu wa wizara ya uchumi wa buluu na uvuvi. Anasema lengo kuu la wizara hiyo ni utekelezaji wa agenda nzima ya uchumi wa buluu hapa visiwani Zanzibar.

Anasema Agenda ya uchumi wa buluu imegawanyika katika maeneo makuu matano.maeneo hayo ni pamoja na .utalii endelevu,uvuvi na mazao ya baharini ikiwemo sekta ya mwani,usafiri wa baharini,Nishati( nishati mbadala pamoja na nishati ya mafuta na Gesi na uendelevu wa miundo mbinu ya kisasa ya nishati pamoja na .usimamizi wa Bahari"Ocean governance"au "blue economy Governance"na suala hili limegawanyijka katika maeneo mbalimbali ikiwemo:

* Uhifadhi wa Bahari
* Rasilimali za Bahari na Mali Asili
* Taarifa za kisayansi utafiti za uvuvi na mali asili za baharini.
* Utekelezaji wa mikataba ya kikanda na ya kimataifa inayohusiana na masuala ya Bahari na suala zima la mabadiliko ya Tabia ya nchi.
* Na masuala mengine ya shirika la kimataifa la usafri wa Baharini.

Vile vile , anasema Wizara ya Uchumi wa buluu ina maeneo makuu 3 ya kijasiliamali na kibiashara ambayo ni Uvuvi wa maji madogo na uvuvi wa bahari kuu,Kilimo cha mwani na Ufugaji wa matango bahari na ufugaji wa kaa
Katibu huyo anasema Tanzanani ni moja kati ya nchi kumi ambazo huzalisha zao la mwani.anasema," mwani ni zao muhimu katika utekelezaji wa madawa bidhaa mbalimbali za manukato,mwani pia ni chakula na masuala mbalimbali ya kiviwandana Bidhaa nyingine za vyakula na tiba.

Anasema Uwezeshaji wa sekta ya matango bahari au majongoo bahari. .hii ni bidhaa ambayo inatumika sana Mashariki ya mbali.majongoo bahari yanauzwa sana katika nchi ya china , hongkong. Korea na Japan.

Anaeleza Wizara hii inajishugulisha sana na maendeleo ya sekta ya kaa .kaa wanasoko kubwa upande wa mashariki ya mbali.

Akizungumzia eneo kuu la pili ambalo wizara inasimamia ni Taasisi ya mafuta na Gas anasema wanazo taasisi mbili zinazo simamamia masuala ya mafuta na Gas.Ambazo ni taasisi inayosimamia uchimbaji na usimamizi wa mafuta na gas(ZPRA) pamoja na Uchimbaji na maendeleo ya mafuta na gas (ZPDC).

Pia eneo kuu la tatu ni usimamizi wa bahari.uhifadhi wa maeneo yote ya bahari.ni wajibu kufanya utafiti Zaidi wa bahari na kukusanya taarifa nyingi za bahari. Ili kuhakikisha rasilimali za bahari zinatuletea faida kubwa kwa maslahi ya taifa na wananchi.

Akizungumzia Majukukumu ya wizara ya uchumi wa buluu na uvuvi anasema ,"usimamizi na utekelezaji wa mikataba ya bahari( mikaataba ya uvuvi na mabadiliko ya hali ya nchi ,kuhakikisha bahari inatumika kisheria,Kupambana na magendo ya madawa ya kulevya,Utayari wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi"

Anasema Wizara ya uchumi wa buluu imepata mafanikio makubwa katikaUzalishaji wa mazao ya bahari pamoja na Utoaji wa fursa za uwekezaji Kufikia mwaka 2023 tayari wamezalisha tani 47,110 za samaki kupitia mradi wa "ahueni uviko 2019".anasema watazalisha tani 55,000 kufikia mwisho wa mwaka huu.

Mafanikio mengine ni Uvuvi endelevu unaojali fursa na jamii. Wizara hii ilikuwa ikizalisha Tani 30 za matango bahari. Sasa tuna uwezekano wa kuzalisha tani 40 mpk mwisho wa mwaka 2023.

Anasema Pia ilikuwa ikizalisha Tani 177 za kaa kuzalisha na kusafirisha na wanaweza kufuikia tani 360 kufikia 2023 yote ni kwaajili ya mafanikio ya ,Mheshimiwa Raisi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr Hussein Ali Mwinyi.

Anasema Utekelezaji wa miundo mbinu ya madagaa. Wamefanikiwa kupeleka dagaa congo Rwanda Burundi na ulaya magharibi Zaidi ya tani 3500 za madagaa kufikia mwaka 2020 -2021.Lengo ni kuwa na dagaa safi na bora tunaweza kuzalisha mara mbili zaidi.

Mafanikio mengine ni mlango mmoja wa kufikia ubora wa mazao wa bahari katika kuzidisha na kupanua wigo kupitia idara ya uvuvi Tanzania bara na Zanzibar.Huu ni mchango mkubwa uliofanywa na Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimia Samia Suluhu Hassan.

Katika eneo la mafuta na gas wamepiga hatua za utafutaji wa taarifa za data ambazo itasaidia Zanzibar kupitia wizara ya nishati Tanzania Bara,pia wizara hii nashirikiana na wadau mbalimbali katika mafunzo na uwezeshaji wa kitaalamu.

Katibu huyo anasema Wizara ya uchumi wa buluu inatotolesha vifaranga vya matango bahari kaa na samaki pamoja na Kuanzishisha mashamba ya samaki ndani ya bahari.

Anasema Pia zipo changamoto ambazo zinaikabili wizara hii ikiwemo:Wananchi bado wanahitaji kupewa elimu na uelewa.ni changamoto ambayo inatakiwa kufanyiwa kazi kila siku.

Akizungumzia Changamoto nyingine ni Teknolojia.Pia Mitaji ,bila mitaji huwezi kupanga( mitaji midogo, na ya kimataifa pamoja na mitaji ya kibank na mitaji ya ndani. Inakuja kwa njia ya uwekezaji na kuwawezesha wananchi. Lakini kampeni ya " Ahueni uviko 19" imeweza kuwawapeleka mbele wavuvi na wananchi kwa ujumla.

Anasema Changamoto kubwa ni Masoko na ubunifu. Ukizalisha sana ni lazima uwe na masoko ya uhakika. Ni moja ya changamoto ambayo serikali inafutia ufumbuzi Vile vile ,Anasema Katika changamoto ya Miundombinu, ifikapo tarehe 10 januari 2023 wizara hii itafungua diko la soko la samaki la malindi.

Anasema Wizara ya uchumi wa buluu kupitia Mpango wa maendeleo ya Zanzibar kufikia 2025 wamejipanga asilimia 60% ya ajira itokane na uchumi wa buluu.

Pia kufikia 2025 asilimia 60% ya pato la taifa liwe limetokea katka sekta ya uchumi wa buluu Pia Kuhakikisha pato la taifa linapanda kutoka 4.9% mpk kufikia asilimia 10% na kuendelea mbele.

Mpango mwingine ni uendeshaji wa bandari mpya ya manga pwani,." Mangapwani multipurpose port complex"

Akizungumzia Matarijio yao ya baadae ni kuipita nchi ya Madagascar ambayo ndiyo mzalishaji mkubwa wa matango bahari ulimwenguni kote.

# MAADHIMISHO YA MIAKA 59 YA MAPINDUZI MATUKUFU YA ZANZIBAR




**59** MIAKA YA MAPINDUZI

17225902

Uongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar inaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi** pamoja na wananchi wote katika kuadhimisha miaka 59 ya mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya 1964.

**"MAPINDUZI DAIMA"**



Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan



## Walalamika kukosa majisafi na salama kwa miaka 20

**Na Dege Masoli,** MUHEZA

WANANCHI wa Kitongoji cha Vanga kilichoko Kata ya Mlingano, Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, wamelalamika kutembea umbali mrefu kutafuta maji kutokana na eneo hilo kukosa huduma hiyo kwa zaidi ya miongo miwili sasa.

Kutokana na tatizo hilo, wakazi hao wanalazimika kuhemea maji ya kunywa pamoja na matumizi ya nyumbani katika maeneo hatari ya Mto Mkurumuzi, ambayo siyo salama kwa matumizi ya binadamu.

Kwa nyakati tofauti jana na juzi, wananchi hao akiwamo Mwantuamu Hamza, alisema licha ya kuyafuata maji hayo mtoni, bado mto huo uko umbali wa kilomita nne kutoka kilipo kitongoji hicho.

"Kwa mateso tunayoyapata hasa wanawake na watoto, kufuata maji mtoni licha ya kuwapo wanyama wakali kama mamba, tunaiomba serikali kuja na ufumbuzi wa kudumu wa adha hii.

"Tunajua Waziri wa Maji, Jumaa Aweso na Mbunge wa Muheza, Hamisi Mwinjuma (Mwana FA) wanatusikia. Tumelalamika ngazi mbalimbali lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa, huku tukiendelea kutumia maji hayo."

Anna Sangali, alisema kuwa huduma ya maji wanayoipata siyo salama na kwamba kutokana na umbali huo, inawawia vigumu kutekeleza kwa wakati mipango yao ya maendeleo na hivyo kuwa kikwazo kwao cha kiuchumi.

Juma Ramadhan alisema waliwahi kupata maji ya bomba kutoka katika Mradi wa Maji wa Pongwe, jijini Tanga, uliokuwa ukipeleka maji kwenye Chuo cha Utafiti cha Mlingano, lakini maji hayo kwa sasa hayafiki katika kitongoji hicho.

Alipotafutwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Tanga, Geofrey Hill, alisema kuwa tayari kitongoji hicho na vingine vipo kwenye mpango wa kupatiwa maji.

Mwanzoni mwa mwezi huu, Mbunge wa Muheza (CCM), Hamisi Mwinjuma, alitangaza ujio wa neema hiyo, akisema mchakato wa kumaliza tatizo la uhaba wa maji ya bomba katika Wilaya ya Muheza, uko ukingoni baada ya serikali kukusudia kuja na mradi mpya utakaogharimu Sh. bilioni 40.

# Prof. Mkenda atengua katazo matumizi ya Kiswahili shuleni

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, amesitisha marufuku iliyowekwa katika Mkoa wa Mara ya kuzuia matumizi ya lugha ya Kiswahili shuleni.

Amesema ameondoa marufuku hiyo hadi wanafunzi walioingia kidato cha kwanza mwaka huu wamalize wiki nane za kujifunza na kuzungumza kwa ufasaha lugha ya Kiingereza.

Jana Prof. Mkenda alisema tayari ameshazungumza na kumshauri Mkuu wa Mkoa wa Mara (Meja Jenerali, Suleiman Mzee) na kumshauri wasitishe na kutafuta ubunifu mwingine.

"Kuna mkoa mmoja, ofisa wake, amesema wanafunzi wetu wakimaliza darasa la saba na wakiingia sekondari, inabidi kwanza wakae wajifunze lugha, kabla hawajaanza masomo.

"Nimeongea na Mkuu wa Mkoa wa Mara, nimemshauri, tusitishe tutafute ubunifu mwingine, lakini mwarobaini wake utakuja kupitia mapitio ya sera na mitaala mipya.

Zaidi aliongeza: "Lakini tunaelewa kabisa tatizo hilo lililoko la kuwafundisha watoto, darasa la nne, la sita na la saba. Unafundisha Kiingereza unamaliza hawezi kuongea Kiingereza. Hiyo siyo dalili tu kwamba hatufundishi vizuri, tuna kazi kubwa ya ku-improve kufundisha."

Uamuzi wa Waziri huyo wa Elimu, unatokana na amri iliyotolewa na ofisa mmoja wa Mkoa wa Mara, aliyenukuliwa katika mkanda wa video akisema,

"Katika kuimarisha taaluma, tumetoa maelekezo kwamba Mkoa wa Mara, kuanzia tarehe 9 Januari wanafunzi wote ambao wataanza kidato cha kwanza, wataanza na 'English Orientation' kwa kipindi cha wiki nane.

"Na tutawa-test wanafunzi wale (tutawapima), hakuna kusoma masomo ya kawaida, watafanya English Orientation, baada ya wiki nane tuta-watest wanafunzi, tutajua viwango vyao vya uelewa wa Kiingereza.

"Na la tatu katika hilo, tumepiga marufuku lugha ya Kiswahili kutumika kwenye shule zetu zote za sekondari.

"Tunahitaji tuhakikishe kuwa wanafunzi wanamudu lugha ya Kiingereza kama ambavyo Sera ya Elimu na Sheria ya Elimu inavyoelekeza. Tumebaini kuwa lugha ile inasababisha wanafunzi wengi wanafeli kwa sababu hawamudu kujieleza," alisisitiza.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (wa tatu kushoto), akikagua orodha ya wanafunzi wapya kwenye Shule ya Sekondari Simanjiro, baada ya kutembelea shule mbalimbali akiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Bilioni 100/- zatengwa ujenzi wa vyuo vya mafunzo ya ufundi

**Na Anjela Mhando,** MWANGA

MIRADI 63 ya ujenzi wa vyuo vipya vya mafunzo ya ufundi stadi nchini imetengewa Sh. bilioni 100, huku serikali ikieleza kuwa tayari makandarasi zaidi ya 50 wamejitokeza kuomba kutekeleza miradi hiyo.

Akizungumzia miradi hiyo akiwa Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, aliwahimiza makandarasi wengine na kampuni za ujenzi kujitokeza kuomba kazi hizo.

"Serikali inayo azma ya kujenga vyuo vya ufundi stadi katika kila mkoa na wilaya hapa nchini. Sasa kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023, tumetenga kiasi hicho cha fedha ni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika wilaya 63, ambazo zilikuwa hazijatengwa vyuo hivyo,"alisema.

Desemba 21, mwaka jana, Prof. Mkenda, aliiagiza menejimenti ya VETA kuhakikisha ujenzi wa vyuo hivyo uwe umeanza mwishoni mwa Januari mwaka huu.

"Wilaya ya Mwanga ni miongoni mwa wilaya 63 ambazo zipo kwenye mpango wa kujengewa Chuo cha Ufundi Stadi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

"Nimpongeze Mbunge wa Mwanga, Joseph Tadayo, kwa jitihada zake kubwa za kuweza kufanikisha upatikanaji wa hati ya ardhi itakapojengwa chuo hicho.

"Kazi kubwa imefanywa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kufanikisha kutapatikana eneo lenye ukubwa wa ekari 50 zilizopo katika Kitongoji cha Kisangiro, ambapo chuo hicho kitajengwa.

Awali Mbunge wa Mwanga, Joseph Tadayo, alisema ujio wa chuo hicho utapunguza tatizo la ajira kwa vijana, kwa kuwa kitawawezesha vijana wanapohitimu elimu ya msingi, kidato cha nne na kuendelea kujiunga na chuo hicho. Alisema pia wataweza kujifunza kazi mbalimbali ili waweze kujiajiri, badala ya kusubiri kuajiriwa.

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdallah Mwaipaya, alisema kiwanja hicho kimesajiliwa kwa namba 161502 na kwamba kiwanja hicho kina hati miliki namba 67119 ya miaka 99.



HABARI KANDA YA ZIWA

# Walalamika kutolipwa fidia ya maeneo kufunikwa na tope

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAKAZI wa vijiji vya Ng'wanholo na Nyenze wilayani Kishapu wamelalamikia kuchelewa kulipwa fidia ya maeneo yao ikiwamo nyumba na mashamba ambayo yalifunikwa na tope kutoka Mgodi wa Almasi wa Mwadui.

Wananchi hao walipaza kilio hicho juzi kwa Meneja Mkuu wa mgodi huo, Ayoub Mwenda, wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na wananchi waliotaka kufahamu lini watalipwa fidia zao.

Mmoja wa wananchi hao, Elias Mabele, alisema tangu litokee janga hilo la tope la mgodi kufunika mali zao Novemba 7 mwaka jana, hakuna kinachoendelea hadi sasa juu ya hatima ya kulipwa fidia na hawana maeneo ya kulima tena katika msimu huu wa kilimo.

"Meneja tunashukuru umesikia wito wetu na kuja kutusikiliza tangu litokee janga la bwawa la mgodi la kuhifadhia maji machafu Novemba 7, mwaka jana na kutuathiri maeneo yetu ikiwamo nyumba kufunikiwa na tope na mashamba, swali letu lini tunalipwa fidia?" Alisema Mabele.

Mkazi mwingine, Ester Nguli, alilalamikia kitendo cha baadhi ya wataalamu ambao wanapita kufanya tathmini kuwa wamekuwa wakipunguza idadi ya mali ambazo wamepoteza ikiwamo mashamba na kuuomba uongozi wa mgodi huo utende haki ili wananchi walipwe fidia inayostahili.

Kuhusu kuhamia katika maeneo elekezi, wakazi hao walisema hawatakwenda kuishi katika maeneo yoyote ambayo wanasikia tu kupitia vyombo vya habari kueleza kuwa hawawezi kwenda kuishi huko kienyeji kwa sababu hawajashirikishwa.

Meneja Mkuu wa mgodi huo, Mwenda, aliwatoa wasiwasi wananchi hao akisema haki itatendeka na hakuna mwananchi hata mmoja ambaye hatolipwa fidia, huku akiwaomba wawe na subira wakati taratibu za tathmini zikiendelea.

Aidha, aliwataka wananchi ambao wanalalamika kutotendewa haki juu ya taratibu za tathmini ikiwamo kupunguziwa ukubwa wa mashamba yao, wafike kwenye mgodi huo ili wafanyiwe upya uthamini na kupata haki zao kwa mujibu wa sheria.

Novemba 7, mwaka jana, bwawa la kuhifadhia maji machafu katika mgodi huo lilibomoka na tope zito kuvamia makazi ya watu na kufunika nyumba, visima vya maji pamoja na mashamba.



Meneja Mkuu wa Mgodi wa Almasi wa Williamson Diamond Ltd wa Mwadui, Mhandisi Ayoub Mwenda, akizungumza na wananchi wa vijiji vya Ng'wanholo na Nyenze, Kata ya Mwadui Luhumbo, wilayani Kishapu juzi, ambao ni waathirika wa tope la bwawa la kuhifadhia maji machafu la mgodi huo, lilipobomoka Novemba 7 mwaka jana, akiwataka kuwa na subira wakati taratibu za tathmini zikiendelea kwa ajili ya kuwalipa fidia. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Walimu mahiri wa Kiingereza kutumika kufundisha wanafunzi

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

SERIKALI ya Mkoa wa Kagera imesema wameshatoa maelekezo kwa wakuu wa shule za sekondari kuwapangia majukumu walimu mahiri katika lugha ya Kiingereza ambao watawafundisha wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Elimu Sekondari mkoani humo, Khalifa Shemahonge, alisema licha ya lugha hiyo kuwa ya kufundishia bado imekuwa kaa la moto kwa wanafunzi wanaojifungua na elimu hiyo ya upili.

"Lengo ni kutatua tatizo hili la lugha ya Kiingereza kwa sababu mtoto akiweza kupata umahiri katika lugha hiyo ana uwezo wa kusoma fizikia, kemia, uraia na masomo mengine na kuelewa vizuri na ni rahisi hata kujisomea mwenyewe kwa sababu atakuwa anaelewa," alisema.

Shemahonge alisema uteuzi wa walimu hao mahiri katika lugha hiyo ni utekelezaji wa baadhi ya maelekezo yaliyotolewa katika kikao cha maofisa elimu wote katika mkoa huo.

Aidha, alisema kuwa mbali na maelekezo hayo mkakati mwingine ni maofisa elimu kata, wakuu wa shule za sekondari na walimu wakuu wa shule za msingi kuhakikisha wanawabaini watoto waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, kufahamu wanapoishi ili ambao watashindwa kuripoti wasakwe.

Aliwataka wazazi kutimiza wajibu wao kwa kuhakikisha wanawapeleka watoto shule bila kuwachelewesha ili wasiachwe katika masomo.

Alisema: "Shule zimefunguliwa tangu Januari 09 mwaka huu, ombi langu kwa wazazi, watoto wasichelewe, wakichelewa wataachwa katika masomo hata wakijitahidi kuwafikia wenzao itakuwa vigumu maana mkianza safari pamoja mtamaliza pamoja."

# H'shauri yatenga mil.100/- kukabili mfumuko wa bei

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imetenga Sh. milioni 100 kwa ajili ya kukabiliana na mfumuko wa bei ya vyakula.

Hivyo wamewawezesha pembejeo za ruzuku za kilimo wakulima vijana wenye uwezo wa kulima mazao ya chakula na biashara kuanzia hekari tano na kuendelea.

Akitoa ufafanuzi wa hali ya bei ya unga wa mahindi, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kahama, Anderson Msumba, alisema imepanda kutoka Sh.1,500 hadi Sh.2,200 kwa kilo moja.

Alisema Kahama haijitoshelezi kwa chakula kwa maana ya uzalishaji hali ambayo inafanya vyakula kutoka mikoa jirani.

Msumba alisema kila mwaka halmashauri imekuwa ikitenga Sh.milioni 70 na kununua pembejeo za ruzuku na kuzigawa bure kwa wakulima vijana wenye uwezo wa kulima ekari tano na kuendelea za mazao ya chakula na biashara.

Alisema mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga Sh.milioni 100 za ruzuku za kilimo na mazao wanayopata ni mali ya wazalishaji.

Msumba alisema manispaa hiyo inazalisha kwa wingi mpunga, mahindi na pamba kwa uchache, huku mpunga ukizalishwa kwa asilimia 89 na mahindi asilimia 97, hekari zinazofaa katika kilimo zikiwa 180, 532 na zinazoliwa na wakulima ni hekari 156,187.5 sawa na asilimia 86.6 na zilizobaki zimeishia kuwa sehemu ya makazi ya watu.

Kadhalika, alisema katika kuhakikisha uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara yanaongezeka wamewezesha maofisa ugani waliopo kila kata usafiri wa kuwawezesha kuwafikia wakulima na kuwashauri namna ya kulima kisasa. Alisema na hivi karibuni serikali imeongeza vitendea kazi na mashine za kupima udogo ili kujua aina gani ya mazao inatakiwa kulimwa.

"Utoaji wa pembejeo za ruzuku kupitia fedha za mapato ya ndani ya halmashauri yetu ni fursa kwa vijana kuzalisha zaidi mazao ya chakula na biashara na sisi tutaendelea kuwashika mikono kupitia asilimia 10 ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ikiwa na bei hutegemea na upatikanaji wa bidhaa husika,"alisema Msumba.

Mmoja wa wakulima vijana, Agness Ezekiel alisema utaratibu uliofanywa na halmashauri ya kutoa pembejeo kwa wakulima vijana imesaidia kuondoa vijana mitaani waliohitimu masomo yao na kubaki kutegemea ajira kutoka serikalini.

Alisema kulingana na mabadiliko ya tabianchi ni vema wakawekeza zaidi kwenye kilimo chenye tija hususani mazao yanayohimiri hali ya ukame.

Mkulima mwingine, Lonar Masawe alisema upandaji wa bei ya vyakula inategemeana na uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu, hivyo kwa utoaji wa pembejeo za ruzuku utasaidia kuondoa mfumko wa bei hususani katika unga wa mahindi kwani kwa sasa wananunua kilo moja kwa Sh. 2,500 kutoka Sh.1,500.



# Miaka 59 ya mapinduzi Zanzibar

ALHAMISI JANUARI 12, 2023

TOLEO MAALUM

**Na Mwandishi Wetu**

# Chimbuko la Zanzibar, mapinduzi yake, ilikojikita mzizi wa asili yake

LEO Wazanzibari na raia wote wa Tanzania, wanasherehekea kumbukumbu ya 'Mapinduzi Matukufu' nchini, ikitimu mwaka wa 59.

Hata hivyo, inapochimbwa mzizi wa makazi katika kisiwa hicho inagota hadi mzizi wa miaka 20,000 kumekuwapo makazi ya binadamu, katika visiwa vya Zanzibar.

Kupitia historia hizo, inaanzia pale wafanyabiashara wa Kiajemi walivigundua visiwa hivyo na kuvifanya makao makuu, kwa safari kati ya Mashariki ya Kati, India na Afrika.


Katika kipindi walianza biashara na Waarabu waliofika Afrika ya Mashariki na ilipofika kwenye Karne ya Saba, Waarabu walifika Zanzibar kibiashara, pamoja na kusambaza imani ya dini ya Uislamu; ndio walioipa jina la Zanzibar, kutokana na maneno ya Kiajemi 'Zinjibar' .

Pia, ilipofika Karne ya 13, lugha ya Kiswahili ilianza kutumika na ni zao la mchanganyiko wa lugha ya Kiarabu na Kiafrika.

Hata ilipofika Karne 16, Zanzibar ilipata umaarufu zaidi kibiashara na hata kupata ugeni wa Wareno, huku biashara ya Utumwa ikichukua nafasi, lakini kukawepo hali ya uongozi wa mahali hapo na ukionekana ukiingiliwa.

Waarabu kutoka Oman walichukua utawala Zanzibar katika Karne ya 17 na Zanzibar ikawa makao makuu ya Utawala wa Waomani.

Safari ilisonga wastani wa miaka 50, kati ya miaka ya 1820 na1870, Zanzibar ilifaidika kiuchumi, ikawa na maendeleo yaliyosababishwa na utawala wa Masultani huku imani ya Kiislamu nayo ikimea kwa kasi.



Marehemu Rais wa kwanza wa Zanzibar, Abeid Aman Karume. **PICHA: MAKTABA.**

Hadi inapogota mwaka wa 1830, Zanzibar ilinawiri katika kilimo cha karafuu na haja kubwa ya kuwapo wazalishaji shamba la watumwa na inatajwa kufika wakati Watumwa ndio wakaunda sehemu kubwa ya wakazi wote.

Ikiegemea mgawanyo wa dunia wa mkutano wa Berlin, Ujerumani wa mwaka 1884 hadi 1885, Kamisheni kutoka Uingereza na Ujerumani, mwaka 1885 ikaamua kuigawa Zanzibar kutoka katika utawala wa Kisultani na ndio ukawa mwisho wa utawala wa kujitegemea Zanzibar. Mnamo mwaka 1886, Sultani akafikia maridhiano hayo.

Mwaka 1890 Zanzibar ilikuwa chini ya uangalizi wa Waingereza rasmi na uchaguzi wa mwanzo ulifanyika mwaka 1957, hata hivyo inaelezwa

miaka iliyofuata, kukawepo fujo na machafuko kutoka kwa Waafrika wanaodai uhuru dhidi ya utawala wa Kiarabu.

Mwezi Desemba mwaka 1963 Waingereza waliipa uhuru Zanzibar chini ya jumuiya ya madola.

**ILIVYOKUWA MAPINDUZI**

Tarehe 12 Januari 1964, Zanzibar ilifanya mapinduzi kujikomboa kutoka katika utawala wa sultani.

Muda mchache baadaye iliungana na Tanganyika kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mapinduzi ya Zanzibar yalitokea mwaka 1964, ili kumuondoa madarakani Sultani wa Zanzibar na serikali yake, iliyoundwa hasa na Waarabu.

Hatimaye, ikaweka uongozi mikononi mwa Waafrika, ambao ndio wengi visiwani humo (230,000 hivi), kwenye bahari ya Hindi, karibu na pwani ya Tanganyika.

Usultani wa Zanzibar ulikuwa umepewa na Uingereza uhuru wake mwaka 1963. Kabla ya hapo, Waarabu walikuwa wamefaulu kudumisha katika mfululizo wa chaguzi utawala waliokuwa nao tangu zamani za Zanzibar kuwa chini ya Usultani wa Omani.

Chama cha Afro-Shirazi Party (ASP), kilichowakilisha hasa Waafrika, kilipoona kwamba bungeni kina viti vichache ingawa kilipata asilimia 54 za kura katika uchaguzi wa Julai 1963, kilipatana na chama cha mrengo wa kushoto Umma Party.

Tarehe 12 Januari 1964 asubuhi na mapema, mwanachama wa ASP John Okello, ambaye alikuwa na asili kutoka Uganda( mzaliwa wa 1937-1971 ) aliongoza wanamapinduzi 600 hadi 800 wa kisiwa kikuu cha Unguja kuishinda polisi wa nchi na kuteka silaha zao.

Halafu wakaelekea mjini Zanzibar walipompindua Sultani Jamshid bin Abdullah na serikali yake. Inakadiriwa waliokufa walikuwa 80.

Kilichofuata kwa siku kadhaa kukawepo na msukosuko wa kiusalama na hali ikatengemaa, kiongozi wa chama ASP, Abeid Karume, akapewa nafasi serikalini.

Mwelekeo wa Kikomunisti wa baadhi katika serikali mpya uliogopesha nchi za Magharibi. Kwa kuwa Zanzibar ilikuwa chini ya athari ya Uingereza, serikali yake iliandaa mipango kadhaa. Hata hivyo, hofu ya kuundwa serikali ya Kikomunisti haikutimia kamwe, na kwa kuwa wananchi wa Uingereza na Marekani waliweza kuhama bila shida, mipango hiyo haikutekelezwa.

Wakati huo nchi za Kikomunisti za China, Ujerumani Mashariki na Umoja wa Kisovyeti zilianzisha uhusiano wa kirafiki na serikali mpya ya Zanzibar, kwa kuitambua rasmi na kutuma washauri.

Karume alifanikisha majadiliano ya kuunganisha Zanzibar na Tanganyika, ili kuunda hatimaye muungano wa Tanzania Aprili 1964.

Ni mapinduzi yaliyokomesha miaka 200 ya utawala wa Waarabu Zanzibar, na ndiyo leo ni sehemu ya maadhimisho ya mapinduzi Zanzibar.

# Kutoka hoteli mbili za 1964 hadi 600 za 2023

• Utalii umekamata theluthi ya uchumi; idadi ya ndege na wageni inatia fora

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MIAKA 59 tangu kufanyika Mapinduzi mwaka 1964 ambayo ni miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana Zanzibar, kumeshuhudiwa kuimarika mambo kadhaa.

Hapo inaingia katika rekodi, sekta ya utalii na ikineemeka kwa namna yake, kukitajwa mageuzi kutoka hoteli mbili mwaka 1964 hadi 600 mwaka ulioisha.

Kuimarika huko kwa sekta hiyo, kunatajwa kunatokana na sababu mbalimbali, ikiwamo hali ya amani na utulivu iliyopo visiwani humo ikikaribisha uwekezaji Visiwani, sekta hiyo ikiingizia serikali mapato kwa asilimia 21.

Hadi sasa, kunatajwa ujio wa wageni kwa kasi kutoka mataifa mbalimbali duniani, wanaofika kwa shughuli mbalimbali, pia kikuu mapumziko, fukwe zikiwa sehemu ya vivutio vikubwa.

ANENAVYO DK. SHEIN

Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk Ali Muhammed Shein, anataja baada ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), kulikuwapo hoteli alizozitaja kwa majina; Afrika House na Zanzibar Hotel, lakini sasa kuna hoteli nyingi za kitalii, ikiwajengea Wazanzibari hali ya kujivunia.

Pia, ni wakala wa mabadiliko na mageuzi zaidi katika sekta ya utalii na serikali ikiwa na jukumu kubwa la kufanikisha kuongeza ujenzi wa hoteli zaidi.

Dk. Shein anasema, kumekuwapo jitihada za kujenga hoteli baada ya Mapinduzi Zanzibar, zilianza mwaka 1970 kwa kujenga hoteli ya Bwawani na hoteli tatu Pemba; Hoteli ya Mkoani, Chakechake na Wete, ndipo harakati zikapamba moto kuukaribisha utalii.

Kwa mujibu wa Dk Shein, mwaka 2013 ni rais, aliandaa mpango mkubwa wa utalii ulioitwa 'Utalii kwa Wote' ili kila mwananchi wa Zanzibar awe na haki kupata tija, faraja na maendeleo kuhusu utalii.

Anasema baada ya hapo idadi ya watalii ikazidi kuongezeka kutoka mwaka 1986, akitaja kulikuwapo watalii 29,211 hadi mwaka 2019 kufikisha watalii 588,264.

"Kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo maambukizi ya UVIKO-19, yalitupa mtihani mkubwa sana idadi yetu ya watalii ilishuka sana kutoka watalii 538,000 hadi kufika 339,000 na mapato yetu ya utalii yalipungua sana," anasema.

Anafafanua kuwa, mbali na changamoto hizo, serikali ikajitahidi Zanzibar ikapata afuweni ya uchumi na kuimarisha uchumi wake na hadi kufikia mwaka jana, watalii walianza kuongezeka, akirejea takwimu za Oktoba mwaka jana, watalii waliofika



RAIS Mstaafu wa Zanzibar, Dk Ali Mohammed Shein, akisalimiana na Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hafsa Mbamba, katika hafla ya uzinduzi wa Hoteli ya Toa, iliyopo Pongwe Mkoa wa Kusini Unguja. **PICHA. RAHMA SULEIMAN.**

Zanzibar walikuwa 425,908.

Anasema hadi sasa, utalii ndio sekta mama ya uchumi wa Zanzibar, hivyo sekta zote zinapaswa kuhakikisha zinaisadia sekta hiyo na utalii na nchi zenye visiwa utalii ndio unaoimarisha uchumi wake.

**BAADA YA UVIKO**

Baada ya janga la UVIKO-19 kupungua, idadi ya watalii ikaanza kuongezeka, mwaka 2022 wakiwa watalii 487,031 waliingia Zanzibar kwa kutumia usafiri wa anga.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, mwaka jana kulikuwapo safari za ndege 15,347 hali inayoiwezesha mamlaka hiyo kukusanya mapato shilingi bilioni 8.135 (Sh. 8,135,052,467.76).

Pia, ikirejewa takwimu za mwaka mmoja kabla, 2021 mamlaka hiyo ilikusanya shilingi bilioni 4.858 (Sh.4, 858,523,843.50), wakati wageni waliongia katika viwanja vya ndege walikuwa 328,196 na safari za ndege zilikuwa 12,321.

Mwaka mmoja kabla, 2020 zilikusanya mapato ya shilingi bilioni 2.588 (Sh. 2,585,957,329.38), wageni walikuwa 235,597 na safari za ndege 11,066.



Hoteli iliyopo majini kisiwani Pemba.

**HALI YA UTALII**

Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hapsa Hassan Mbamba, anasema Sekta ya Utalii imebaki kinara wa kuingiza fedha nyingi za kigeni katika uchumi wa visiwa hivyo vya Zanzibar.

Anasema, kiasi cha asilimia 80 ya fedha za kigeni zinatokana na Sekta ya Utalii, huku ikimiliki asilimia 29.2 ya uchumi wa Zanzibar.

Mbamba anasema, wakati wa kipindi cha misukosuko ya maradhi ya Uviko -19, kabla ya ujio wa wageni visiwani ilishuka, kufikia 260,644, hata hivyo Zanzibar haikufunga mipaka yake.

Katibu Mtendaji huyo anasema, mwaka 2021 wageni walioingia Zanzibar walikuwa 364,185 lakini mwaka jana hadi Novemba walikuwa 322,748.

Anasema malengo ya serikali ni kwamba, ifikapo mwaka 2025, iwe inaingiza zaidi wageni wa kitalii, wastani 800,000 na kinachofanyika sasa ni kwamba serikali inajipanga kuhakikisha kutangaza utalii katika nchi mbalimbali, hasa kupitia wageni wanaofanya mikutano yao Zanzibar .

Mbamba anasema kwa kuwa sekta ya utalii ni mtambuka, nao wamejipanga, katika kuhakikisha wanatumia michezo ikiwamo ya baharini, ili kuwavuta zaidi wageni.

"Tunataka watalii wenye uwezo wa kifedha kwa ajili ya manunuzi mbalimbali, ili serikali iongeze pato litokanalo na sekta hii ya utalii," anasema Mbamba.

Hapo anafafanua kuwa, utafiti uliofanywa umeonyesha kuwa watalii wengi wanaofika Zanzibar, hutembelea fukwe na sio kufanya utalii wa vyanzo vingine vya utalii.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo, inasema mwaka jana kati ya Januari hadi Novemba, jumla ya wageni 52,666 walitembelea hifadhi hiyo na kuchangia kuingiza zaidi ya shilingi bilioni 1.19 huku fedha za kigeni zilizokuswanywa zikiwa zaidi ya dola 68,000.

Mwaka 2021, jumla ya wageni 58,902 waliotembelea hifadhi hiyo na kuingiza kiasi cha shilingi bilioni 1.56, ikiwa ni ada za kiingilio katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka huo.

**UTALII MIRADI MIKUBWA**

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwezekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar, (ZIPA) Sharif Ali Sharif, anawataka wazanzibari kusoma ili kupata ajira katika miradi ya uwekezaji ikiwamo, utalii ili ajira hizo zisichukuliwe na wageni.

Anasema, SMZ kupitia ZIPA, ina mipango yake ikiwamo kuwa na sera na sheria mpya ya uwekezaji, itakayokuwa rafiki katika kusimamia masuala ya uwekezaji, katika hali ya kisasa ikiwamo huduma kwa kidigitali.

Anasema katika kipindi kifupi wamesajili miradi yenye thamani ya dola bilioni tatu ambayo inatarajia kutoa ajira zaidi ya 13,000 kwa wananchi wa Zanzibar.

"Wakati tukisherehekea maadhimisho ya miaka 59 ya mapinduzi haya ndio yaliyokusudiwa kuhakikisha wananchi wa visiwa vyetu wanagomboka, sio kisiasa hata kiuchumi na kunufaika na rasilimali za taifa lao, uwekezaji ni sehemu kubwa ya uchumi"anasema.

Anasema, katika kuhakikisha wawekezaji wanafika kuwekeza Zanzibar, miradi mbalimbali imeshaonesha njia ambapo visiwa 17 wawekezaji wameonyesha nia ya kuwekeza, ikiwamo visiwa vya Mnemba , Misali Pemba na jumla ya dola milioni 414.50 zitapatikana.

Anasema pia serikali itapata dola milioni 213.16 kwa ajili ya miradi ya



Mandhari ya hoteli na ufukwe wa Unguja.



Ndege zikiwa zimeegeshwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume, Unguja. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

hoteli 30 na dola milioni 18.26 miradi tisa ambapo miradi hiyo tayari imeshasajiliwa na ZIPA.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Yusuph Juma Mwenda, anasema mapato wanayokusanywa zaidi ya asilimia 50 yanatokana na sekta ya utalii.

Anawataka wanaofanya kazi za watembeza watalii wajisajili ili kulipa kodi ambayo itaiwezesha serikali kuwaletea maendeleo wananchi na kupeleka mbele gurudumu la maendeleo kupitia sekta hiyo.

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR**

# MAFANIKIO YA SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR NA MIAKA 59 YA MAPINDUZI

Shirika la umeme Zanzibar (ZECO) lilianzishwa kwa sheria no 3 ya mwaka 2006.lakini kabla ya hapo lilikuwa likijulikana kama shirika la mafuta na nguvu za umeme lilianzishwa wakati wa mapinduzi ya mwaka 1964.

Katika kusherekea maadhimisho ya miaka 59 ya sherehe za mapinduzi tunaendelea kushuhudia mafanikio makubwa tangu serikali ya mapinduzi ya awamu ya nane inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi ilipoingia madarakani. Katika serikali hii ya awamu ya nane kupitia ilani ya chama cha mapinduzi kabla ya kufikia 2025 serikali kupitia shirika la umeme Zanzibar(zeco) litaingiza kwa mara ya kwanza uzalishaji wa umeme chanzo cha uzalishaji wa umeme kwa mara ya kwanza kupitia nishati ya jua.

Meneja mkuu wa shirika la umeme Zanzibar, Dk,Ndugu Mshenga Haidar Mshenga anasema,"Lengo kuu la kuanzishwa shirika hilo ni kuzalisha , kusafirisha na kusambaza pamoja na kuuza umeme kwa wananchi. Jukumu lingine la ziada la shirika la umeme Zanzibar ni kuhakikisha linachochea maendeleo katika taasisi zingine. Kwa njia ya kupeleka huduma za umeme.

Anasema pia ,Mpaka kufikia miaka 59 ya mapinduzi matukufu ya Zanzibar, shirika la umeme Zanzibar (zeco) imeshafikisha huduma ya umeme kwa asilimia 90% katika miji ya unguja na pemba.yaliyobaki ni matoleo tu ya vijiji ambavyo vinaongezeka.

Anasema Katika sekta ya umeme maendeleo yanapimwa kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya umeme.miaka ya 1980 waya wa umeme kutokea shirika la umeme Tanzania( Tanesco )ulikuwa na uwezo wa mega watt 45 kufikia 2010 waya huu ulijaa kutokana na kuzidiwa uwezo.serikali ililazimika kuweka waya mwingine wa Mega watt 100 . mpaka kufikia mwaka 2023 waya huu umeshatumika asilimia 90% Anasema piaChangamoto kubwa ya shirika la umeme Zanzibar(zeco) ni madeni kwani watu wengi waliokuwa wanatumia metre waliacha madeni japokuwa changamoto imetatuliwa kwa sehemu na matumizi ya metre za Tukuza.

Vilevile anasema kuwa changamoto nyingine ambayo inaikabili shirika la umeme Zanzibar ni wizi wa umeme kwa wananchi ambao siyo waaminifu.inasababisha serikali kupoteza mapato.

Akizungumzia changamoto nyingine ni uwezo wa shirika kiujumla katika kuwahudumia wananchi.huduma zimepanda lakini uwezo wa kuwahudumia wananchi umekuwa ni mdogo. Watu wengi wanasubiri huduma.
Anasema Matarajio ya baadae ni kuhakikisha wanatoa huduma bora na kwa ufanisi Zaidi.

Aidha Ametoa rai kwa jamii kushirikiana na shirika hilo katika kulinda miundombinu ya shirika la umeme zeco .Anasema" kulinda miundombinu ni uzalendo.pia kulipa gharama za umeme ni uzalendo .unapokosesha mapato unalidhoofisha shirika.

**"ZECO TUNANG'ARISHA MAISHA YAKO."**

## MAADHIMISHO YA MIAKA 59 YA MAPINDUZI MATUKUFU YA ZANZIBAR




Uongozi na Wafanyakazi wote wa Sirika la Umeme Zanzibar inaungana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi** pamoja na wananchi wote katika kuadhimisha miaka 59 ya mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya 1964.

**"MAPINDUZI DAIMA"**

Gulioni Street Zanizbar P.O.BOX: 235 Zanzibar
Telephone: +255 2452255 (Head Office). +255 2452259
(Pemba). Contact us · External links · STAFF MAIL.

17226002

## SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR

**59**

***Ya Mapinduzi***



***Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi***



***Sheikh Abedi Amani Karume***

***Bodi ya wakurugenzi, Mkurugenzi Mtendaji na wafanyakazi wote wa Shirika la Nyumba Zanziba ZHC tunaungana na Raisi wa Zanziba na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi Zanzibar ya 1964.***

***"MAPINDUZI DAIMA"***

217226202

+255 242230067 www.zhc.go.tz info@zhc.go.tz zhczanzibar Nyumba bora kwa Maendeleo ya Zanzibar

## MAFANIKIO YA SHIRIKA LA NYUMBA NA MIAKA 59 YA MAPINDUZI

Shirika la Nyumba Zanzibar ni Taasisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayojitegemea ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa sheria namba 6 ya mwaka 2014 .Shirika la Nyumba Zanzibar limepewa mamlaka ya kusimamia na kuendeleza sekta ya nyumba Zanzibar.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la nyumba Zanzibar Mwanaisha Ali Said anasema, Malengo waliyojiwekea Shirika la Nyumba Zanzibar ni pamoja na kuhakikisha kupatikana kwa ujenzi bora, imara na viwango vya juu vilivyokusudiwa.

Pia anasema Katika kuhakikisha suala hilo Shirika la Nyumba Zanzibar limekuwa likifanya ukaguzi na ufuatiliaji wa mradi wa matengenezo ya majengo yaliyopo visiwani Unguja na Pemba.

Katika kuelekea kilele cha kuadhimisha miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar,Shirika la Nyumba Zanzibar linampongeza Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa mchango wake mkubwa katika kuboresha majengo ya kisasa na yenye ubora.

**Mafanikio ya shirika la nyumba Zanzibar ni pamoja na:**

- Kuanzishwa kwa miradi ya ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Biashara ikiwemo Mombasa kwa Unguja na Mabatini, Kilimatinde Chake Chake kwa upande wa Pemba
- Kupangishwa kwa nyumba za Shirika
- Kufuatilia malipo ya kodi na madeni yote ya nyumba za Shirika
- Kufanya matengenezo kwa nyumba za Maendeleo zikiwemo nyumba za Michenzani bloki 01 kwa Upande wa Unguja, Madungu, Mtemani na Wete kwa upande wa Pemba na nyumba zisizo za maendeleo zikiwemo Nyumba ya Malindi Mabanda ya Papa, Nyumba ya Mkunazini Darajani Mnadani, Nyumba ya Mji Mkongwe Dizenga

Mkurugenzi huyo pia amesema Changamoto kubwa inayolikabili Shirika la Nyumba Zanzibar ni baadhi ya wapangaji kutokuwa waaminifu kwa kuuza nyumba za Shirika kwa watu wengine wakati wao wakiwa wamekodishwa.

Changamoto nyingine ni baadhi ya wapangaji wa Shirika kulimbikiza madeni yao. Tabia hii inapelekea ucheleweshwaji wa mapato ya serikali.
Pia Changamoto nyingine ni baadhi ya wapangaji kufanya nyumba za kulaza wageni pamoja madanguro na vituo vya madawa .

Pia wapangaji kuweka dhamana kwa kutumia nyumba za shirika.
Mkurugenzi huyo amesema ili kuweza kutatua changamoto sheria limejiwekea utaratibu wa kukagua miradi ,maeneo na nyumba za shirika.

Lakini pia anasema pindi wanapoona wapangajiwamechelewesha malipo huwapatia kwanza barua kali za onyo.ikiwa ni pamoja na kuzifunga nyumba hizo pindi wapangaji hao wanapokiuka mikataba iliyowekwa na Shirika.

Pia anasema Shirika limejiwekea utaratibu wa kutoa elimu kwa vitendo vinavyofundisha utekelezaji wa mikakati ya shirika hilo.
Mkurugenzi anawaomba wateja wote wa Shirika kufuata taratibu zilizowekwa na kutokuvunja sheria .kuhusiana na tabia ya kuuza nyumba za shirika maarufu kama kiremba,Amewataka wapangaji wote wasome mikataba kwa makini.lakini pia wawe na mikataba halali .Aidha shirika litaendelea kuchukua hatua kali dhidi ya mwananchi yeyote atakayegundulika kuvunja taratibu na masharti ya upangishwaji wa nyumba za shirika.

/ / / / / / / / / / / / / /

**"NYUMBA BORA KWA MAENDELEO YA ZANZIBAR"**



# Waziri: Uchomaji misitu chanzo cha uharibifu wa mazingira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, amesema moja kati ya sababu zinazoharibu mazingira nchini ni uchomaji wa misitu unaotokana na shughuli za kibinadamu katika maeneo ya hifadhi za misitu.

Alibainisha hayo jana jijini hapo wakati wa upandaji miti ikiwa ni sehemu ya kuelekea kuadhimisha miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema uharibifu wa mazingira licha ya kuathiri sekta ya utalii umekuwa na madhara makubwa katika shughuli mbalimbali za kila siku za wananchi.

"Uchomaji wa misitu umekuwa moto kwelikweli misitu inaunguzwa hali ambayo inasababisha kuharibu mazingira na kuongezeka kwa athari za mabadiliko tabianchi,"alisema Balozi Chana.

Aidha alisema sababu kuu ya uchomaji wa moto misitu ni wananchi wakati wa kuaanda mashamba, hivyo moto unaotumika kuruka na kwenda katika maeneo mengine ya hifadhi ya misitu.

"Uchomaji moto misitu siyo jambo sahihi wananchi tunapaswa kutafuta namna nyingine ya kuandaa mashamba, siyo kuchoma moto kwa kuwa tunaathiri sana misitu yetu ambayo inatupatia mvua na kuondokana na ukame ambao umekuwa ukitutesa katika sekta ya maji na umeme," alisema.

Kadhalika, alipiga marufuku uingizaji wa mifugo kwenye misitu ili kuepuka uharibifu wa mazingira.

"Tunatakiwa kuilinda na kuitunza misitu kwa sheria zetu ni marufuku mtu yeyote kuingiza mifugo katika misitu hii tuliyonayo ili tuilinde itupatie mvua na kuondokana na athari za mabadiliko tabianchi," alisema.

Alisema kama watu wataendelea kuharibu mazingira ukame utaendelea kuisumbua nchi na kushindwa kufikia malengo yake ambayo imejiwekea katika miradi mbalimbali.

"Hata bwawa la kufua umeme la Mto Rufiji kupitia mradi wa Mwalimu Nyerere tutashinda kulijaza maji kama ambavyo tumejiwekea kwa kuwa hatutakuwa na mvua za kutosha za kujaza maji katika mradi huu," alisisitiza.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Abdallah Mitawi, alisema maagizo yote yaliyotolewa na waziri watahakikisha wanayafanyia kazi ili kulinda mazingira.

Akizungumzia kuhusu upandaji miti katika maadhimisho ya Sikukuu ya Mapinduzi Zanzibar, Mitawi alisema wanatarajia kupata miti 5,300 kwa muda wa siku tatu zilizopangwa.

Hata hivyo aliwataka wakazi wa Mkoa wa Dodoma kujitokeza kwa wingi leo kumuunga mkono Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, atakapoongoza upandaji miti maeneo mbalimbali ya Jiji hilo.



Askari wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Kikosi cha 834 Makutupora, wakipanda miti eneo la CBE, jijini Dodoma jana, ikiwa ni mkakati wa kulifanya jiji hilo kuwa la kijani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Serikali yaagiza elimu bima ya afya kwa wote kutolewa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeagiza kutolewa elimu kwa umma kuhusu mpango wa bima ya afya kwa wote wakati huu ambao muswada ukitarajiwa kwenda kusomwa bungeni.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, alibainisha hayo jana jijini hapa, katika kikao maalumu kati ya Wizara ya Afya na watendaji wakuu wa taasisi zilizoko chini yake ili washiriki kikamilifu katika utoaji elimu kwa wananchi kwa lengo la kuongeza uelewa.

Prof. Makubi, alisema kuwa suala la utoaji elimu hiyo ni mtambuka na lazima kushirikisha wizara na taasisi zingine za serikali na binafsi.

"Tumeandaa mpango harakishi na shirikishi ambao utawahusisha viongozi wote wa wizara nyingi za serikali na taasisi zake na dhamira mahususi ya mpango huo ni kuongeza uelewa na hamasa kwa wananchi kuhusu uelewa wa mambo muhimu yatakayotekelezwa baada ya sheria inayopendekezwa kutungwa," alisema Prof. Makubi.

Aidha, aliwahimiza watendaji hao kwenda kushirikiana na ofisi za wakuu wa mikoa, wilaya ili kutoa elimu ya dhana ya bima ya afya kwa wote.

"Ni muhimu kuyafikia makundi ya wananchi wa kawaida ikiwa ni pamoja na wafanyabiashara, vyama vya ushirika, wakulima, wafugaji, viongozi wa dini, serikali za mitaa, mama ntilie, machinga na bodaboda.

"Tunawafikia kwa kuwapa elimu lengo kubwa ni kuwaomba wakapande mbegu na kutoa elimu zaidi ili kulifikia kundi kubwa la wananchi wenye kuwa na elimu kuhusu dhana na umuhimu wa kujiunga na bima ya afya kwa wote," alisisitiza Prof. Makubi.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliwasilisha bungeni kwa mara ya kwanza Septemba mwaka jana Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote.

# Prof. Ndalichako ataka utoaji maoni Sera ya Vijana uendane na usasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amelitaka Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo kutoa maoni yanayoendana na mahitaji ya sasa kwenye Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2023, ili iwe na tija kwa kundi hilo.

Prof. Ndalichako alitoa wito huo jana jijini hapo alipokuwa akifungua mkutano wa baraza hilo ambao pamoja na mambo mengine ulijadili na kutoa maoni kuhusu sera hiyo.

Alisema vijana ndiyo nguzo ya maendeleo ya taifa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na mambo mengine, jukumu lake kubwa ni kusimamia masuala ya vijana nchini.

"Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2021 inaonesha kuwa kundi la vijana kati ya miaka 15 hadi 35 linajumuisha watu wapatao milioni 20.73 sawa na asilimia 34.9 ya watu wote.

"Hili ni kundi muhimu katika kuleta maendeleo ya nchi yetu, vijana wanapaswa kujengewa misingi ya kulinda amani, umoja na kuendeleza mshikamano katika taifa letu," alisema.

Aidha, alisema maandalizi ya kuandaa Sera ya Maendeleo ya Vijana bado yanaendelea na hatua kadhaa zimeshakamilika ikiwa pamoja na kufanya tathmini ya Sera ya mwaka 2007, kuandaa Rasimu ya Sera ya Mwaka 2023.

Akizungumzia kuhusu mabadiliko ya teknolojia na utandawazi, Prof. Ndalichako alisema mfumo wa maisha duniani umebadilika sana ikiwamo makuzi na tabia ya vijana.

"Tuangalie ni kwa namna gani vijana wetu watanufaika na fursa zinazotokana na maendeleo ya teknolojia. Ni namna gani wanaweza kutumia maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kama fursa ya kuwapatia ajira na kipato,"alisema.

Awali Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Prof. Jamal Katundu, alimhakikishia Waziri Ndalichako kuwa sera hiyo itakamilika ili itumike kwa maendeleo ya vijana nchini.





# Mama mbaroni tuhuma kumuua mtoto wake

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia, Joyce Matingo (26), mkazi wa Unyamwanga Wilaya ya Rungwe kwa tuhuma za kumuua mtoto wake, Emily Matingo (9) kwa kumpiga sehemu mbalimbali za mwili.

Kamanda wa Polisi Mkoani Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi ACP, Benjamin Kuzaga, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa tukio hilo lilitokea Januari 8, mwaka huu majira ya saa 12 jioni.

Alisema mtuhumiwa alimfunga kamba mikono na miguu mtoto wake na kuanza kumchapa fimbo sehemu mbalimbali za mwili wake na kusababisha kifo chake.

"Mwanafaunzi huyo alikuwa akisoma darasa la tatu katika Shule ya Msingi Unyamwanga wilayani Rungwe na kwamba aliuawa na mama yake akituhumiwa kuiba pesa shilingi 16,000 awamu ya kwanza na shilingi 40,000 awamu ya pili zilizokuwa zimehifadhiwa ndani," alisema ACP Kuzaga.

Kutokana na hali hiyo, alitoa wito kwa wazazi na walezi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu zilizopitiliza na kusababisha madhara makubwa.

Alisema jamii inapaswa kuwalea watoto katika maadili mazuri ili kuwaepusha na tabia mbaya ikiwamo wizi.

Mratibu wa Dawati la Jinsia Mkoa wa Mbeya, Loveness Mtemi, alisema asilimia kubwa ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vinafanywa na wazazi au walezi wao.

Alisema wanapokea matukio mengi ya ukatili kutoka kwa watoto na kwamba wanapofuatilia wanabaini wazazi ndiyo wanaohusika, hivyo aliiomba jamii kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi na badala yake wafuate sheria.




Mwanafunzi wa Shule Maalum ya Msingi Katumba II, Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, Glory Mwambungu (kushoto), akiwasilisha mada kuhusu haki mbalimbali za watoto wenye ulemavu wakiwamo wenye ualbino, katika hafla ya kumaliza mradi wa kuboresha mazingira salama na jumuishi kwa watoto wote nchini ulioratibiwa na Shirika la Kuhudumia Watoto wenye Ulemavu Tanzania (CST), wilayani humo juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TANROADS yaagizwa kuweka mzani Igawa-Uwanja wa Ndege Songwe

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BODI ya Barabara Mkoa wa Mbeya imeuagiza Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) mkoani humo kuweka mzani kwenye Barabara Kuu ya TANZAM kuanzia eneo la Igawa mpaka Uwanja wa Ndege wa Songwe ili kuzuia uharibifu wa barabara.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa kauli hiyo juzi kwenye kikao cha Bodi ya Barabara.

Alisema kumekuwa na uharibifu wa barabara kwenye kipande hicho hali inayohatarisha usalama wa vyombo vya usafiri na abiria.

Alisema kwa sasa malori mengi yanabeba mizigo mingi na mikubwa hali inayosababisha uharibifu wa barabara, hivyo ipo haja kwa TANROADS kujenga mizani kuanzia eneo la Igawa mpaka Uwanja wa Ndege wa Songwe.

"Kuna haja ya kujenga mizani kwenye kipande cha barabara kuanzia eneo la Igawa liliko wilayani Mbarali mpaka Uwanja wa Ndege wa Songwe ili kuepukana na uharibifu wa barabara ambayo inahatarisha maisha ni muhimu sana maagizo haya yakatekelezwa haraka kwa sababu wote tumejionea hali halisi ya barabara hiyo," alisema Homera.

Meneja TANROADS Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Matari Masige, alisema tatizo la kuharibika kwa barabara wanalifahamu na kwamba wameanzisha mradi ambao utajenga mizani ili kuepusha uharibifu wa barabara.

"Kwa sasa kuna mizani iliyoko eneo la Uyole ambayo inaelekea Barabara ya Kasumulu lakini mizani hiyo itajengwa haraka na kwamba kuna mizani nyingine mkoani Songwe ya Mpemba ambayo inasaidia kukabiliana na tatizo hilo," Mhandisi Masige.

Baadhi ya wajumbe wa Bodi ya Barabara akiwamo Mbunge wa Chunya, Masache Kasaka alisema kipande cha barabara kuanzia Igawa mpaka Uwanja wa Songwe siyo rafiki kwa sababu ya kuharibiwa na magari ya mizigo.

Hivyo aliunga mkono ujenzi wa mizani ikiwa ni sehemu ya kutunza na kuhifadhi barabara ambayo ni tegemeo kwa shughuli za uchumi.

# Wilaya ya Chunya yaongoza kwa tatizo la udumavu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

OFISA lishe wa Mkoa wa Mbeya, Benson Sanga, amesema Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya inaongoza kwa tatizo la udumavu ambao unasababishwa na lishe duni.

Kwa mujibu wa Sanga Wilaya ya Chunya ina asilimia 32 ukilinganisha na kiwango cha mkoa ambacho ni asilimia 22.9.

Alisema kutokana na hali hiyo wameanza jitihada za kutekeleza afua za lishe ili kukabiliana na tatizo la udumavu kwa Wilaya za Chunya na Mbeya ambazo zina tatizo hilo kwa kiasi kikubwa.

Alisema Mkoa wa Mbeya unatoa elimu ya lishe kwa jamii ili kuongeza uelewa na kubadili tabia ya ulaji ikiwa ni hatua ya kukabiliana na hali ya udumavu.

Alisema wanatoa elimu hiyo kupitia majukwaa ya kijamii na klabu za lishe shuleni, kwamba hadi sasa ni asilimia 87.9 ya shule za msingi na sekondari zimeanzisha.

Alidai kuwa kila halmashauri imekuwa ikisimamia utekelezaji wa siku ya afya na lishe ya kijiji ambayo huandaliwa na wanakijiji na mahitaji ya vyakula vinavyohitajika kwa ajili ya utoaji wa elimu ya lishe kwa nadharia na vitendo.

"Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ina asilimia 32 ya udumavu, Wilaya ya Mbeya (31), Jiji la Mbeya, (26), Mbarali (21), Rungwe (18) na Kyela (13) ambapo hata hivyo mkoa umekuwa ukiratibu ufuatiliaji wa hali ya lishe ya watoto chini ya miaka mitano na kufanikiwa kufikisha asilimia 33.8," alisema Sanga.

Aliongeza kuwa afua za lishe katika ngazi ya kata zote 179 za Mkoa wa Mbeya zimeteua waratibu wa lishe ambao husimamia utekelezaji wa afua za lishe pamoja na kuwasimamia wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

Alisema hali ya lishe kwa watu wazima imeweza kutambuliwa kupitia majukwaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na maadhimisho ya magonjwa yasiyoambukiza, kwamba wanawake wenye uzito uliozidi ni asilimia 21 na wanaume ni asilimia 25.

Alisema wanawake wenye uzito pungufu ni asilimia 3.4 huku wanaume ni asilimia 3.1 na wanawake wajawazito wenye upungufu wa damu ni asilimia 26.



## Dk. Mwinyi ataka wavuvi wawezeshwe vifaa vya kisasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema lazima wavuvi wawezeshwe kwa kupatiwa vifaa vya kisasa na meli za kuvulia ili waweze kuvua samaki wengi na wakubwa.

Aliyasema hayo juzi wakati wa hafla ya ufunguzi wa Soko la Samaki Malindi Mjini Unguja ikiwa ni maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Alisema wakati serikali inazungumzia uchumi wa buluu lazima kuwawezesha wavuvi kuwa na vifaa vya kisasa vya uvuvi na ikipendeza kila mkoa kuwa na soko la kisasa la kuuzia samaki.

Alisema masoko kama hayo yanawawezesha wavuvi kupata kipato kikubwa kwa sababu kuna vyumba maalum vya baridi kwa ajili ya kuhifadhia samaki.

Alisema haiwezekani wavuvi wanakwenda baharini kutafuta samaki lakini hulazimika kuwauza kwa bei ndogo kwa sababu wakibaki hawana pa kuwahifadhi.

"Uchumi wa buluu tunauzungumzia ndio huu kuwa na masoko kama haya, vyumba baridi vya kuhifadhia samaki, mitambo ya kutengenezea barafu na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi lazima kuhakikisha kila mkoa kuna soko kama hili,"alisema.

Aidha, alisema lazima kuwa na viwanda vya kuchakata samaki ili kuuza nje ya nchi na wavuvi kuwa na soko la uhakika.

Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, aliwataka watendaji wanaosimamia soko kuhakikisha wanalitunza na kuliendeleza na wasipokuwa makini soko hilo litaharibika.

Alisema usafi ni muhimu katika soko hilo, hivyo aliwaomba viongozi kuondoa muhali katika suala hilo na kuweka nguvu za pamoja kutafuta mtu ambaye atalisimamia.

Hivyo, aliitaka Serikali ya Mkoa na Manispaa kulisimamia ili liendelee kuwa safi na kudumu kwa muda mrefu. Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema ujenzi huo ulichukua miezi 18, ulijumuisha ujenzi wa bandari ya maegesho ya boti, jengo jipya la soko, ofisi, ukarabati wa jengo la zamani, miundombinu ya kuhifadhia samaki na mtambo wa kuzalisha barafu.

Alisema mradi huo umetekelezwa na Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Kimaendeleo la Japan (JAICA) na lengo la mradi huo ni kuwawezesha watu wanaotumia soko la samaki kuuza na kununua samaki wakiwa katika hali ya usalama.

Alisema ujenzi huo wa soko umegharimu Dola za Marekani milioni 14.7 na lina vyumba vya kuhifadhia samaki vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 200.

# Jeshi la Polisi lahadharisha maofisa wake kuhusu mikutano ya siasa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, amewahadharisha maofisa, wakaguzi na askari wa Jeshi la Polisi Kamisheni ya Zanzibar kusimamia kikamilifu jukumu la kuweka ulinzi na usalama na kutokua kikwazo katika mikutano ya vyama vya siasa.

Alitoa tahadhari hiyo jana wakati akizungumza na maofisa, wakaguzi wa Jeshi la Polisi.

Alisema jukumu la Jeshi la Polisi katika mikutano hiyo ni kuweka ulinzi na usalama na lisitumike kuwa chanzo cha kusababisha migogoro.

Hivyo, aliwataka kuepuka kutumia nguvu zisizo za lazima endapo kutatokea migongano na badala yake watumie busara na hekima ili mikutano hiyo ifanyike bila ya kuvunja sheria za nchi.

Aidha, aliwataka makamanda wa mikoa kujipanga kimkakati katika ngazi zote kwa lengo la kuhakikisha usimamizi wa mikutano ya hadhara inafanyika kwa amani na utulivu.

"Itakapobainika kuna uvunjifu wa sheria iwe kwa vitendo au maneno, hatua zichukuliwe kwa wahusika kwa namna ambayo haiwezi kusababisha uvunjifu wa sheria au amani iliyoko," alisema.

Alisema jeshi hilo limeunda madawati maalum yatakayohusika kufuatilia mwenendo wa mikutano hiyo ili ifanyike kwa kufuata sheria na taratibu za nchi.

Pia aliwataka askari hao kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na kuepuka mihemko au kujiingiza katika makundi ya siasa ya upande wowote, kuepuka kutoa lugha za kejeli na atakayebainika hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

Alisema milango ya Jeshi la Polisi iko wazi kushirikiana na vyama vya siasa, taasisi, pamoja na wananchi ili kuhakikisha amani iliyoko inaendelea kudumu.

Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Zuberi Chembera, alisema utii wa sheria kwa viongozi wa vyama vya siasa na watendaji wa Jeshi la Polisi pamoja na ushirikiano wa karibu yatasaidia kuondoa migogoro baina ya pande hizo na kufanyika kwa mikutano hiyo katika hali ya utulivu.

Alisema kila upande unapaswa kutimiza wajibu wake na endapo patatokea tatizo lolote la kisiasa au la kiusalama vyama vya siasa vinapaswa kukaa pamoja na Jeshi la Polisi kutatua.

Aidha, aliwataka wanasiasa kutotumia vibaya fursa hiyo iliotolewa na Rais Samia na badala yake waitumie vizuri na endapo ukifanyika ukiukwaji wa sheria na taratibu hatua za kisheria zitachukuliwa.




Wasanii wa Kikundi cha Ocean Art cha Mwanakwerekwe, Unguja, wakifanya igizo la uchumi wa buluu, wakati wa ufunguzi wa Diko na Soko la Samaki Malindizi, Wilaya ya Mjini Unguja juzi. **PICHA: IKULU**

# Samia: Mapinduzi ya Zanzibar yameleta neema, ukombozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amesema Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 yameleta neema na kumkomboa Mzanzibari kwa sababu kabla ya mapinduzi hayo kulikuwa na shule 68 pekee.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua shule mpya ya msingi iliyopewa jina lake iliyoko Mwanakwerekwe Mjini Zanzibar, kwamba ujenzi wa shule hiyo umetokana na fedha za UVIKO-19.

Alisema kati ya shule hizo za msingi 62, sekondari tano na maandalizi moja na kwa wakati huo idadi ya wanafunzi ilikuwa 24,000 kwa shule ya msingi na 1,000 kwa sekondari.

Alisema pamoja na uwapo wa shule hizo lakini mtoto wa mnyonge wa kizanzibar hakupata fursa ya kwenda kwenye shule hizo kwa sababu maeneo mengi ya Zanzibar hakukuwa na shule.

Alisema baada ya Mapinduzi ya Zanzibar zikaanza kujengwa shule lakini kwa sasa maendeleo yamesababisha kuwapo kwa shule za ghorofa zenye hadhi nzuri.

Rais Samia alisema katika kuhakikisha wananchi wote wanapata haki yao ya elimu, baada ya Mapinduzi ya Zanzibar serikali imeamua kuweka fedha nyingi katika elimu ili kuimarisha miundombinu ya shule na kukuza ubora wa elimu.

Alisema kuna ongezeko kubwa la watoto kwa sababu Wazanzibari wameongezeka na mahitaji ya sekta ya jamii nayo yamekuwa makubwa.

"Tutaendelea kuimarisha miundombinu ya shule kulingana na mahitaji ya ongezeko la watu ili kuhakikisha hakuna mtoto wa kitanzania anayekosa kuingia darasani na serikali itahakikisha mazingira bora ya kujifunza na kufundishia kwa kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani," alisema Rais Samia.

Rais Samia alisema ugonjwa wa corona umeleta balaa lakini umeleta neema kwa wale waliotumia akili na serikali imekopa fedha kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) na fedha hizo zimetumika katika miradi ya maendeleo ikiwamo maji, afya na elimu.

"Kwa upande wetu Tanzania fedha hizi tumezitumia ipasavyo ni mkopo ambao umeleta manufaa makubwa kwa wananchi, hivyo ndugu zangu mkopo huu unatakiwa kulipwa, tufanye kazi kwa bidii, tulipe kodi zetu tukusanye na tupate kulipa mkopo huu," alisema.

Aidha, alisema ameridhika na miradi ya maendeleo iliyomalizika ambayo inatokana na fedha hizo za corona.

Alisema ni dhambi kubwa kuwa na majengo mazuri ya shule lakini matokeo ya mitihani yakiwa mabaya, hivyo ni vyema matokeo yakaenda sambamba na hadhi ya majengo hayo ya shule huku akiwataka walimu kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Rais Samia alisema watoto lazima watumie teknolojia na kuanza masomo ya sayansi mapema kwa sababu yanapotoka matokeo ya mitahani ya taifa kwa shule za Zanzibar huwa siyo mazuri hivyo watoto wakikuzwa vizuri tokea mapema kutakuwa na wataalamu wazuri.

Pia aliwataka wazazi na walezi kusimamia matumizi mazuri ya simu kwa watoto wao ili kuitumia vizuri teknolojia hiyo ambayo itawawezesha kufanya vizuri katika masomo yao.

Alisema Zanzibar ilifika wakati darasa moja shuleni likiwa na wanafunzi 180 hali ambayo iliwalazimu walimu kuwa na walimu wawili mmoja kazi yake ni kufundisha na mwingine kuwatuliza wanafunzi.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa, alisema jengo hilo la ghorofa moja lina madarasa 29 na ni miongoni mwa majengo 45 mapya ya shule kwamba wizara yake imejenga kupitia fedha za corona na Wizara ya Elimu ilipewa Sh. bilioni 83.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja imejenga madarasa 1,131, vyoo 1,693, madawati 40,000 na seti za viti na meza 35,000.

# Ukraine yaomba vifaru kuikabili Russia

**KYIV, Ukraine**

UKRAINE imeiomba Ujerumani kuipatia zana za kijeshi ikiwamo vifaru vya kisasa ili kukabiliana na mashambulizi ya Russia.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine, Dmytro Kuleba, alitoa ombi hilo kwa waziri mwenzie wa Ujerumani Annalena Baerbock , wakati walipotembelea mji wa Kharkiv juzi.

Hata hivyo, vikosi vya Russia vimeendeleza mashambulizi yake nchini Ukraine, kwa kuulenga mji wa Kharkiv, saa chache baada ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Annalena Baerbock kufanya ziara kwenye mji huo.

Taarifa kuhusu hujuma hizo za vikosi vya Russia zimetolewa na gavana wa mkoa wa Kharkiv, Oleg Synegubov, kupitia mtandao wa Telegram.

Katika taarifa hiyo aliwashauri watu kwenye maeneo ya mji huo kubakia mafichoni akisema wavamizi wanavurumisha tena mabomu.

Hata hivyo, hapakuwa na taarifa ya vifo wala majeruhi kutokana na mashambulizi hayo.

Mji wa Kharkiv umekuwa ukishambuliwa mara kwa mara tangu kuanza kwa vita lakini hivi sasa makabiliano yamehamia upande wa mashariki tangu HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/ukraine-yawasukuma-nyuma-wanajeshi-warusi-kharkiv/a-61753594" vikosi vya Ukraine vilipoukomboa mji huo kutoka mikononi mwa Russia mwishoni mwa mwaka jana.

Katika wiki za karibuni mji wa Kharkiv umekuwa alama ya ushindi wa vikosi vya Ukraine kwenye vita vinavyoendelea nchini humo.

Jumanne mwanadiplomasia mkuu wa Ujerumani, Annalena Baerbock aliutembelea mji huo akiwa pamoja na mwenzake wa Ukraine Dmytro Kuleba.

Alitumia ziara hiyo ya siri kutoa ahadi ya Ujerumani kuipatia msaada zaidi ikiwemo silaha na nyongeza ya fedha ili kufanikisha ununuzi wa vifaa muhimu kwa ajili ya vita.

"Mji wa Kharkiv unadhihirisha jinsi ukombozi ulivyo muhimu na jinsi ilivyo muhimu kuendelea kuleta silaha, kwa sababu kwenye mazungumzo yote iwe ni kwenye hospitali ya watoto, au na wanafunzi, au wanajeshi, mtu anasikia na kuhisi makosa ya kivita na uhalifu dhidi ya binadamu uliotendwa na wanajeshi wa Russia kwenye eneo hili" alisema Baerbock.

Katika ziara hiyo Baerbock, alipeleka msaada wa jenerata na kitita cha fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya mawasiliano kufanikisha upatikanaji wa huduma ya intaneti kwenye mji huo.

Hata hivyo, mwenyeji wake Kuleba, alimwambia Baerbock kuwa Ukraine inatarajia zaidi ya majenereta ya kufua umeme.

Nchi hiyo ingependelea Ujerumani ifikie uamuzi wa kutuma vifaru vya kisasa ambavyo serikali yake imeviomba kwa muda mrefu lakini utawala wa kansela Olaf Scholz bado unajikokota kuvipeleka nchini humo.

"Kwa kukosekana uamuzi hivi sasa, kitu pekee kinachoghadhabisha ni kwamba kadri uamuzi unavyokawia, watu wengi zaidi wanapoteza maisha kutokana na upungufu wa vifaru muhimu kwa jeshi letu." alisema Kuleba.

Licha ya fadhaa iliyoelezwa na mwanadiplomasia huyo wa Ukraine, Baerbock ambaye amekuwa kiongozi wa kwanza wa ngazi ya juu kutoka mataifa ya magharibi kulitembelea jimbo la Kharkiv hakusema lolote juu ya iwapo uamuzi wa kuipatia Ukraine vifaru aina ya Leopard utafikiwa hivi karibuni.

Eneo lingine linaloshuhudia mapambano makali ni kitongoji cha mkoa wa Donetsk kiitwacho Soledar, kinachofahamika kwa uzalishaji mkubwa wa chumvi.

Rais Volodymyr Zelenskyy alisema kwenye maeneo yote hayo karibu kila kitu kimeharibiwa.

***DW***



Mwanamke kikongwe akiwa amekaa kando ya ukuta uliopasuka wa nyumba yake huko Joshimath katika wilaya ya Chamoli nchini Afghanistan jana . **PICHA: AFP**

## Rais mpya Peru achunguzwa

**LIMA, Peru**

MWENDESHA mashtaka mkuu wa Peru, ameanzisha uchunguzi dhidi ya Rais Dina Boluarte na mawaziri wakuu kutokana na mapigano ya wiki kadhaa ambayo yamesababisha vifo vya makumi ya watu.

Maofisa hao wanachunguzwa kwa tuhuma za mauaji ya halaiki, yaliyosababisha madhara nchini humo.

Ghasia zilizuka baada ya aliyekuwa Rais Pedro Castillo, kukamatwa mwezi Desemba kwa kujaribu kulivunja Bunge. Jumatatu, watu 17 walikufa katika mapigano kati ya wafuasi wa Castillo na vikosi vya usalama kusini-mashariki mwa Peru.

Makumi ya wengine walijeruhiwa katika mji wa Juliaca katika siku ambayo ilikuwa mbaya ya ghasia.

Wengi wa walioathirika walionekana kuwa na majeraha ya risasi.

Mamlaka ilishutumu waandamanaji kwa kujaribu kuvamia uwanja wa ndege wa Juliaca na kituo cha polisi cha eneo hilo. Amri ya kutotoka nje kwa usiku mmoja sasa imewekwa katika eneo hilo.

Vurugu hizo mpya nchini Peru zimesababisha vifo vya watu wengi Jumanne. Ofisi ya mwanasheria mkuu ilitangaza uamuzi wake wa kumchunguza Rais Boluarte, pamoja na Waziri Mkuu Alberto Otarola pamoja na mawaziri wa ulinzi na mambo ya ndani.

Rais na mawaziri wake hawajatoa maoni yao hadharani kuhusu suala hilo.

**Mamlaka ilishutumu waandamanaji kwa kujaribu kuvamia uwanja wa ndege wa Juliaca na kituo cha polisi cha eneo hilo. Amri ya kutotoka nje kwa usiku mmoja sasa imewekwa katika eneo hilo.**

# Rwanda yakanusha kuwazuia wakimbizi

**KIGALI, Rwanda**

SIKU chache baada ya Rais wa Rwanda Paul Kagame, kutoa kauli tata kuhusu wakimbizi kutoka DRC kuingia nchini humo, msemaji wa serikali amekanusha Rwanda kutoruhusu wakimbizi kuingia.

Yolande Makolo alisema kuwa vyombo vya habari vimepotosha hotuba ya Rais Kagame.

''Badala ya kushughulikia changamoto ya kuleta usalama na amani katika eneo ambalo raia wake hawastahili chochote, baadhi ya vyombo vya habari vilichagua kupotosha wito wa Rais Kagame wa uongozi na uwajibikaji kuwa ni tishio la kuwafukuza au kuwapiga marufuku wakimbizi'' alisema Yolande katika ukurasa wake wa Twitter.

''Rwanda haina nia ya kuwafukuza au kuwapiga marufuku wakimbizi. Daima tunakaribisha watu wanaokimbia ukosefu wa usalama, mateso na vurugu. Tunaomba jumuiya ya kimataifa ichukue jukumu la kutafuta suluhu la kudumu kwa kundi hili la wakimbizi waliosahaulika kutoka DRC'' Aliongeza Yolande katika taarifa yake.

Katika taarifa yake Rais Kagame alisema Rwanda haiwezi kuendelea kubeba mzigo wa DRC.

"Hili si tatizo la Rwanda," alisema Kagame na kuongeza: "Ninakataa kwamba Rwanda inapaswa kubeba mzigo huu."

Rwanda inashutumiwa kwa kuunga mkono kundi la waasi la M23, jambo ambalo nchi hiyo imekuwa ikikanusha. Kundi hilo la waasi limeteka maeneo mengi katika miezi ya hivi karibuni, na kutuma makumi ya maelfu ya wakimbizi kuvuka mpaka na kuingia Rwanda.

***BBC***

# Mafundi mabingwa Umoja Cup

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Mafundi kutoka Obwere imefanikiwa kutwaa taji la mashindano ya Umoja Cup Rorya 2022 baada ya kuwafunga KMT kwa penalti 4-1.

Mchezo huo uliokuwa mgumu na wenye ushindano ulimalizika kwa suluhu katika dakika 90 za kawaida, lakini dakika ya 60, KMT walipata bao ambalo lilikataliwa na mwamuzi msaidizi ambaye alitafsiri ameotea.

Wachezaji wa KMT wakiongozwa na kocha wao walilalamikia kutokana na kukataliwa kwa goli hilo lakini mwamuzi, Francis Azaria, alisimamia sheria na mechi hiyo ilimalizika kwa kupigwa penalti.

Mabao ya Mafundi yalifungwa na Nasibu Ally, Jerry Odada, Msuva Joseph na Ajele Warioba wakati Mbae Juma alifunga goli pekee la KMT.

Mwenyekiti wa Umoja Cup, Ochieng Melli, akimkaribisha mgeni rasmi alishukuru timu zote zilizoshiriki mashindano hayo pamoja na mdhamini wa mashindano hayo, Peter Owino.



Kikosi cha mabingwa wapya wa mashindano ya Umoja Cup Rorya 2022, Mafundi FC kutoka Obwere. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Mgeni rasmi, Kelvin Mackooko, aliwasisitiza vijana kuendelea kushiriki katika michezo kwa nidhamu ya hali ya juu kwa sababu inasaidia kuongeza ajira.

Mackooko alimkabidhi, Oson Nyando, tuzo ya heshima kwa kutambua mchango wake katika soka wilayani humo.

# SINGIDA BS, MAFUNZO FC ZAJIPANGA KUSHIRIKIANA

**Na Saada Akida, ZANZIBAR**

WAKATI Singida Big Stars ikiendelea na maandalizi kwa ajili ya mchezo wa fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi, uongozi wa timu hiyo umeingia katika makubaliano na mabosi wa Mafunzo FC ya Visiwani hapo kwa ajili ya kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kiufundi kwenye sekta hizo za michezo.

Singida Big Stars itacheza fainali ya mashindano hayo kesho dhidi ya wenyeji Mlandege.

Makubaliano hayo yalifanyika rasmi jana baada ya kikosi cha Singida Big Stars kutembelea gereza la wafungwa la watoto (Chuo cha Mafunzo), kwa ajili ya kutoa misaada mbalimbali ikiwa ni sehemu ya kurudisha shukrani kwa jamii.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Msaidizi wa Singida Big Stars, Muhibu Kanu, alisema malengo makubwa ya ushirikiano huo ni kuendeleza michezo ikiwamo ufundi.

Kanu alisema Singida Big Stars imejipanga kutoa elimu kwa makocha wa Mafunzo pamoja na kuandaa matamasha mbalimbali ya kimichezo.

"Tumeingia makubaliano na uongozi wa Mafunzo FC kwa ajili ya ushirikiano huo pamoja na kutembelea gereza la watoto kwa ajili ya kuwapa zawadi na mahitaji muhimu kama sabuni za kuogea na kufulia," alisema Kanu.

Kamisheni Mkuu wa Chuo cha Mafunzo, Khamis Bakari Khamis, alisema ni jambo zuri kwa uongozi wa klabu hizo mbili na anaamini makubaliano hayo yatasaidia timu yao kupata nafasi ya kujifunza mbinu za kiufundi na michezo.

"Hii ni nafasi kwetu kwa timu ya Mafunzo kurejea katika ubora wake wa miaka ya nyuma kwa sababu tunatarajia makocha wetu watapata vitu vingi vya elimu lakini kwenda Singida kushiriki baadhi ya matamasha yao," alisema Khamis.

Fainali ya Kombe la Mapinduzi itachezwa kesho kwenye Uwanja wa Amaan na bingwa wa michuano hiyo atakabidhiwa kitita cha Sh. milioni 30.

Mabingwa watetezi, Simba waliondolewa mapema katika michuano hiyo pamoja na Yanga, Azam FC, ambazo kwa sasa zimerejea kujiandaa na mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MADRID YAMTAKA KANE

REAL Madrid inataka kumsajili mshambuliaji wa England, Harry Kane kwa ajili ya msimu ujao. Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 huko Tottenham Hotspur unaendelea hadi mwaka 2024 na anaweza kugharimu hadi euro milioni 100. ***(Todofichajes)***

### GERRARD KUINOA POLAND

POLAND imewasiliana na kocha wa zamani wa Rangers na Aston Villa, Steven Gerrard kuhusu kuwa kocha wao mpya. ***(Meczyki)***

### HAZARD ATAJWA ARSENAL

ARSENAL inafikiria kumnunua winga wa Real Madrid, Eden Hazard, mwenye umri wa miaka 32, ambaye alistaafu kucheza soka ya kimataifa akiwa na Ubelgiji Desemba mwaka jana. ***(Mediafoot)***

### CHELSEA, SPURS VITANI

CHELSEA imeungana na Tottenham Hotspur kutaka kumsajili beki wa Hispania, Pedro Porro mwenye umri wa miaka 23, huku klabu yake ya Sporting Lisbon ikitaka kipengele chake cha kuachiliwa cha euro milioni 45 kilipwe chote. ***(90Min)***

### DEPAY KUMRITHI JOAO

KLABU ya Atletico Madrid inamtazama mshambuliaji wa Barcelona, Mholanzi Memphis Depay, mwenye umri wa miaka 28 kama mmoja wa wachezaji wanaoweza kuchukua nafasi ya mchezaji wa kimataifa wa Ureno, Joao Felix (23), ambaye anatazamiwa kujiunga na Chelsea kwa mkopo kwa muda wote uliobaki. ***(sportitalia.com)***

### WEGHORST KUTUA UNITED

KLABU ya Besiktas imekubali kupokea takriban pauni milioni 2.7 kutoka Manchester United ili kumruhusu mshambuliaji wa Uholanzi, Wout Weghorst mwenye umri wa miaka 30 kukatisha mkopo wake kutoka Burnley mapema na kuhamia Old Trafford hadi mwisho wa msimu. Hata hivyo, upande Waturuki hao unataka kupata mbadala wa nyota huyo kabla ya kuruhusu uhamisho wake. ***(Guardian)***

### DANJUMA ANUKIA EVERTON

EVERTON ipo kwenye mazungumzo na Villarreal kuhusu mkataba wa mkopo wa kiungo wa zamani wa Bournemouth, Arnaut Danjuma, mwenye umri wa miaka 25. ***(Bruno Aleman).***

### MOUKOKO KUTUA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inamfuatilia mshambuliaji wa Ujerumani, Youssoufa Moukoko, ambaye pia anasakwa na Chelsea, na wanaweza kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 kwa uhamisho wa bure wakati mkataba wake na Borussia Dortmund utakapokamilika msimu wa joto. ***(Evening Standard)***

### GUENDOUZI ATAKIWA EPL

KIUNGO wa kati wa Marseille na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Matteo Guendouzi mwenye umri wa miaka 23 amepata ofa kutoka klabu moja ya Ligi Kuu England, EPL. ***(L'Equipe)***

### NYOTA MHOLANZI AFUNGUKA

KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Teun Koopmeiners, mwenye umri wa miaka 24 amesema ni "furaha kuona" akihusishwa na Liverpool, lakini "nazingatia 100% Atalanta" na "furaha" kuchezea timu hiyo ya Serie A. ***(Lengo)***

### DAWSON AKARIBIA WOLVES

WOLVES imeongeza nia yao kwa beki wa West Ham, Craig Dawson mwenye umri wa miaka 32 ambaye mkataba wake na Wagonga nyundo unamalizika msimu ujao wa joto. Klabu ya Molineux ilishindwa kumnunua beki huyo wa kati wa Uingereza mwenye umri wa miaka 32. ***(Express & Star)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG AJIPANGA KUIPA UNITED TAJI

## Kocha huyo afunguka na kuongeza hafikirii kumaliza katika Top Four...

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag ameweka malengo yake ya kumaliza ukame wa miaka sita wa Manchester United wa kutotwaa taji lolote baada ya mabao mawili ya Marcus Rashford kuwasaidia kuifunga Charlton Athletic katika robo fainali ya Kombe la EFL, Jumanne.

Akiwa amechukua nafasi ya Antony ambaye aliifungia United kupata bao la kuongoza pale kwenye dimba la Old Trafford, Rashford alifunga mabao mawili dakika za lala salama na kufanikisha ushindi wa magoli 3-0 dhidi ya timu hiyo inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza.

Mabao mawili ya Rashford yaliihakikishia United kufuzu hatua robo fainali, ambao hawajashinda taji lolote kubwa tangu Jose Mourinho alipotwaa Kombe la EFL na Ligi ya Europa mara mbili mwaka 2017.

"Kumaliza kwenye nne bora kwenye Ligi Kuu England sio kipaumbele. La msingi ni kushinda angalau taji," alisemaTen Hag aliiambia Sky Sports.

"Lakini lazima uende mchezo hadi mchezo. Tutaona kitakachotokea, kisha tutajiandaa vyema."

United walipoteza nafasi kadhaa za kumalizia ushindi kabla ya Rashford kuchukua hatua ya kufunga mabao hayo mawili.

"Nina furaha sana. Tulianza mchezo vizuri sana tukiwa na nguvu nzuri na umakini mzuri, na tukawafunga," alisema.

"Tulitengeneza nafasi, nafasi kubwa, kisha tukatengeneza bao zuri. Ni bao la timu, lakini umaliziaji kutoka kwa Antony ulikuwa mzuri.

"Waliweka mshambuliaji mwingine lakini nadhani hatukuruhusu nafasi. Hapo awali, tulikuwa na nafasi. Tulipaswa kumaliza mchezo huu mapema."

United wameshinda kila mechi kati ya sita tangu kumalizika kwa Kombe la Dunia, huku Rashford akifunga katika kila mchezo (jumla ya mabao saba).

Idadi ya mabao 20 ya Rashford katika msimu huu (mabao 15, asisti tano) sasa ni mara mbili ya mchezaji mwenzake wa karibu (Christian Eriksen mwenye mabao 10).

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,065,5
MECHI KALI
FULHAM
VERSUS
CHELSEA
1 | 3.22
X | 3.37
2 | 2.12
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# 'RONALDO HATATUMIKA KUISAIDIA SAUDIA KOMBE LA DUNIA 2030'

**RIYADH, Saudi Arabia**

KLABU mpya ya Cristiano Ronaldo, Al Nassr imesema mkataba wa mchezaji huyo haujumuishi ahadi yoyote ya kuunga mkono ombi la Saudi Arabia kuandaa Kombe la Dunia la mwaka ifikapo mwaka 2030.

Ripoti zilidai Ronaldo atapokea euro milioni 200 kukuza ofa hiyo juu ya mshahara wake wa mwaka wa pauni milioni 177.

Lakini klabu hiyo ilisema mkataba wake "haujumuishi ahadi za zabuni zozote za Kombe la Dunia".

"Lengo lake kuu la Al Nassr ni kufanya kazi na wachezaji wenzake kuisaidia klabu kupata mafanikio," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Nahodha huyo wa Ureno alijiunga na Al Nassr timu hiyo kama mchezaji huru mwezi uliopita baada ya kuondoka Manchester United kutokana na kufanya mahojiano yenye utata.

Atacheza mechi yake ya kwanza ya Al Nassr Januari 22, mwaka huu dhidi ya Ettifaq, lakini kabla ya hapo anaweza kushiriki katika mechi ya maonyesho dhidi ya Paris St-Germain ya Lionel Messi.

Saudi Arabia inaripotiwa kufikiria ombi la kuandaa pamoja Kombe la Dunia la mwaka 2030 na Ugiriki na Misri.

# Felix rasmi kutua Chelsea

**LONDON, England**

JOAO Felix amepewa ruhusa na Atletico Madrid kufanyiwa vipimo vya afya jijini London huku uhamisho wake wa mkopo kwenda Chelsea ukikaribia kukamilika, vyanzo vimeiambia ESPN.

Vyanzo vimeiambia ESPN Felix alisaini mkataba mpya na Atletico hadi mwaka 2027 kabla ya uhamisho huo wa mkopo wa kutua Chelsea, huku klabu zote mbili zikifikia makubaliano.

Vyanzo viliongeza ada ya awali ni euro milioni 11, ingawa chaguo la uhamisho wa kudumu halitajumuishwa katika mpango huo, na Chelsea ndio yenye jukumu la kumlipa mshahara wa Felix.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Atletico, Miguel Angel Gil Marin alipendekeza mwezi uliopita uhusiano wa Felix na Kocha Mkuu, Diego Simeone ulikuwa mbaya na klabu hiyo iko tayari kukubali ahame.

Mshambuliaji huyo alisajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi katika klabu ya Atletico Madrid mwaka 2019 aliposajiliwa kwa thamani ya euro milioni 126 kutoka Benfica.



505,647/-

# AZAM YABAKIA ZANZIBAR IKIJIIMARISHA NA LIGI KUU

**Na Saada Akida, ZANZIBAR**

BAADA ya kuondolewa katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi, kikosi cha Azam FC kimeendelea kuweka kambi yake visiwani hapa kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Tanzania Prisons utakaochezwa Januari 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Wachezaji wa Azam jana asubuhi walianza programu ya mazoezi ya gym baada ya kushindwa kufurukuta mbele ya Singida Big Stars kwenye mchezo wa hatua ya nusu fainali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Azam FC, Kally Ongala, alisema sasa hivi wanatumia muda walionao kujiweka tayari kuwakabili Prisons na baadaye kushusha kikosi imara kwenye mechi ya Kombe la FA.

Kally alisema wameamua kubakia Zanzibar ili kupata nafasi sahihi ya kurekebisha mapungufu waliyoyabaini kabla ya kurejea Dar es Salaam kuendelea na mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tumeona tuendelee kubakia Zanzibar kwa ajili ya kuweka kambi, tunatarajia kucheza mechi za kirafiki na timu za hapa, ili kumpa nafasi kipa wetu mpya, Abdulai Iddrisu, aliyesajiliwa hivi karibuni," alisema Kally.

Kocha huyo aliongeza wamejiondoa katika vita vya ubingwa lakini mipango yao mikubwa ni kuhakikisha wanafanikiwa kumaliza ligi katika nafasi tatu za juu na kutwaa Kombe la Shirikisho.

"Kufikia malengo hayo ni lazima tufanye maandalizi mazuri, kufanyia kazi madhaifu ya kikosi chetu na wachezaji wanafanya yale tunayowaelekeza katika uwanja wa mazoezi na kuhamishia kwenye mechi kwa kutafuta matokeo ya ushindi," alisema kocha huyo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam FC iko katika nafasi ya tatu nyuma ya vinara na mabingwa watetezi, Yanga na Simba.

# FEI TOTO AGOMA

INATOKA UK. 24

Tanzania Bara.

Hata hivyo, Nduruma alisema wanaziomba mamlaka husika kutoa ridhaa kwa kiungo huyo kupata ruhusa ya kujiunga na klabu nyingine ili kulinda kiwango chake wakati kesi yake ikiendelea kusikilizwa huko CAS.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Hadhi na Wachezaji ya TFF, Saidi Soud, alisema walifanikiwa kuwasikiliza wahusika wa pande zote mbili na baada ya kupitia mikataba yao imeonekana Yanga wana haki juu ya mchezaji huyo.

Soud alisema baada ya kuona hilo wamemtaka nyota huyo na Yanga kwenda kukaa pamoja ili kumaliza tofauti zao na kama kuna klabu inahitaji huduma ya Fei Toto wafuate taratibu na kwa sasa Yanga ndiyo yenye kummiliki mchezaji huyo.

"Katika maelezo ya pande zote mbili ya mchezaji na Yanga hakuna sehemu inayoonyesha Azam FC amemrubuni huyo mchezaji na haihusiki kabisa katika kesi ya Fei Toto na klabu yake ya Yanga," alisema Soud.

Mwenyekiti huyo pia alisema kuhusu suala la mshambuliaji wa Yanga, Lazarous Kambole, TFF haimtambui mchezaji huyo kwa sababu sio mali ya Yanga baada ya ITC yake kupelekwa Uganda katika klabu ya Wasiko Giant.

"Mchezaji Kambole hachezei Yanga kwenye ligi yetu, TFF haimtambui kama amechezea Yanga katika Kombe la Mapinduzi haituhusu, mchezaji huyo alihamishwa kwenda Uganda na ligi hapa hakucheza.

Tulifuata taratibu za kumhamisha ili mchezaji Kisinda (Tuisila), akaruhusiwa. Kwa sasa wachezaji wa kimataifa walisomeka 12 na sio 13, ni kweli Yanga walipigania uhuru na hilo halina shaka, ila usajili na uhuru haviingiliani," alisema Mwenyekiti huyo.

Aliongeza TFF ilifuata taratibu zote na kutoa kibali cha Uhamisho cha Kimataifa (ITC) kwa Kambole aliyejiunga na Wasiko Giant. Kuhusu Kambole kutokwenda Uganda na kuendelea kubaki ndani ya Yanga hilo TFF haituhusu kwa sababu tayari hatumtambui, hiyo sio kazi yetu," Soud alisema.

Nipashe lilifanikiwa kuzungumza na mmiliki wa Wakiso Giant, Mussa Atagenda, alisema walikuwa na mpango wa kuhitaji huduma ya mchezaji huyo lakini uongozi wa Yanga haukuwa tayari kuwapatia kama walivyozungumza.

Atagenda alisema waliomba kumsajili Kambole kwa mkopo lakini hawakufanikiwa kupewa mchezaji huyo kama walivyotarajia.

Kwa sasa Yanga inajiandaa kuwakaribisha Ihefu kutoka Mbarali katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumatatu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.




## Mgunda afunguka kuhusu Robertinho

INATOKA UK. 24

Chama, kwa kupata tuzo ya Mchezaji Bora wa Desemba akisema Mzambia huyo anastahili kwa sababu hata ndani ya kikosi amekuwa chachu ya wachezaji wengine kufanya vizuri.

"Ana haki, kipindi nilichokaa Simba, nimeona mchezaji ambaye amekuwa ni chachu ya wengine kufanya vizuri zaidi ni Chama. Ni mchezaji kiongozi, sisemi wengine hawafanyi vyema, ila yeye amesababisha wengi kutaka kufanya vizuri zaidi, " aliongeza.

Kikao cha Kamati ya Tuzo ya TFF, kilichokutana Januari 7, mwaka huu, pamoja na mambo mengine kilimchagua Mgunda kupata tuzo hiyo akiwashinda Nassredine Nabi wa Yanga na Hans van Pluijm wa Singida United.

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/01/23 | 18:00 | Nottingham Forest vs Leicester City | 2.80 | 3.30 | 2.46 |
| 02. 14/01/23 | 18:00 | Wolverhampton Wanderers vs West Ham United | 2.65 | 3.20 | 2.65 |
| 03. 14/01/23 | 18:00 | Luton Town vs West Bromwich Albion | 2.95 | 3.20 | 2.40 |
| 04. 14/01/23 | 18:00 | Preston North End vs Norwich City | 2.95 | 3.25 | 2.38 |
| 05. 14/01/23 | 18:00 | Reading FC vs Queens Park Rangers | 2.46 | 3.25 | 2.80 |
| 06. 14/01/23 | 18:00 | Sunderland AFC vs Swansea City | 2.49 | 3.25 | 2.75 |
| 07. 14/01/23 | 18:00 | DR Congo vs Uganda | 2.39 | 2.75 | 3.45 |
| 08. 14/01/23 | 18:15 | Girona FC vs Sevilla FC | 2.40 | 3.25 | 2.90 |
| 09. 14/01/23 | 20:15 | KAS Eupen vs St. Truidense VV | 2.80 | 3.35 | 2.42 |
| 10. 14/01/23 | 20:45 | FC Volendam vs RKC Waalwijk | 2.65 | 3.50 | 2.46 |
| 11. 14/01/23 | 21:00 | Ivory Coast vs Senegal | 2.85 | 2.95 | 2.65 |
| 12. 14/01/23 | 23:00 | Real Sociedad San Sebastian vs Athletic Bilbao | 2.50 | 3.15 | 2.80 |
| 13. 15/01/23 | 16:00 | Getafe CF vs Espanyol Barcelona | 2.50 | 2.95 | 2.95 |
| 14. 15/01/23 | 16:30 | Go Ahead Eagles vs FC Utrecht | 2.80 | 3.50 | 2.35 |
| 15. 15/01/23 | 17:00 | Angers SCO vs Clermont Foot 63 | 2.42 | 3.40 | 2.75 |
| 16. 15/01/23 | 17:00 | Montpellier HSC vs FC Nantes | 2.45 | 3.40 | 2.70 |
| 17. 15/01/23 | 17:00 | Stade Reims vs OGC Nice | 2.55 | 3.20 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 12/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1847 | Churchill Brothers vs Neroca FC | 1.61 | 3.85 | 4.58 |
| 14:00 | 2095 | Rio Ave U23 vs FC Famalicao U23 | 2.67 | 3.44 | 2.30 |
| 15:00 | 2917 | Apollon 1926 vs Panserraikos | 5.06 | 3.90 | 1.55 |
| 15:30 | 3487 | Al Fateh (KSA) vs Al-Ettifaq | 2.09 | 3.24 | 3.54 |
| 15:30 | 3669 | AL Tai vs Al Taawon | 3.11 | 3.26 | 2.27 |
| 16:15 | 1118 | Al-Sailiya SC vs Al Ahli Doha SC | 2.27 | 3.50 | 2.68 |
| 16:15 | 5005 | AL Wakrah vs Al Arabi Doha SC | 2.48 | 3.40 | 2.48 |
| 16:30 | 1107 | Dinamo Zagreb vs NK Celje | 1.25 | 5.62 | 8.15 |
| 17:00 | 1556 | Doxa Katokopia vs Ethnikos Achnas | 1.92 | 3.40 | 3.50 |
| 17:00 | 3582 | Hyderabad FC vs Chennaiyin FC | 1.55 | 3.98 | 4.86 |
| 18:00 | 1022 | Saudi Arabia vs Oman | 2.92 | 2.97 | 2.38 |
| 18:00 | 2963 | Ghazl EL Mahallah vs Enppi Club | 2.78 | 2.68 | 2.93 |
| 18:00 | 3161 | Atlas U20 vs Mazatlan FC U20 | 1.72 | 3.66 | 4.10 |
| 18:00 | 3529 | Iraq vs Yemen | 1.12 | 6.40 | 18.42 |
| 18:00 | 5565 | Stuttgart vs Sparta Prague | 1.80 | 3.71 | 3.66 |
| 19:00 | 3437 | Hapoel Nir Ramat Hasharon W vs MS Kiryat Gat W | 9.20 | 5.80 | 1.27 |
| 19:00 | 5151 | Finland vs Estonia | 1.94 | 3.48 | 3.88 |
| 20:00 | 1513 | Al Ahly Cairo vs Al Masry Club | 1.45 | 4.28 | 6.56 |
| 20:00 | 4290 | Fiorentina vs Sampdoria | 1.47 | 4.16 | 6.54 |
| 20:45 | 2647 | Heracles Almelo vs GO Ahead Eagles | 2.11 | 3.40 | 3.01 |
| 21:00 | 5578 | Sweden vs Iceland | 1.80 | 3.48 | 4.64 |
| 21:30 | 2214 | AS Tel Aviv University W vs Hapoel Petach-Tikva W | 3.21 | 3.84 | 1.90 |
| 21:30 | 2340 | Ipora GO vs Morrinhos GO | 1.95 | 3.02 | 3.90 |
| 22:00 | 1674 | Groningen vs SV Spakenburg | 1.37 | 4.57 | 6.61 |
| 22:00 | 2273 | Betis vs Barcelona | 5.45 | 4.14 | 1.54 |
| 22:00 | 4674 | Blauw Geel 38 vs Utrecht | 15.55 | 8.55 | 1.09 |
| 22:00 | 5416 | Madrid Ccf W vs Athletic Bilbao W | 1.72 | 3.84 | 3.88 |
| 22:45 | 1266 | Union Saint Gilloise vs KAA Gent | 2.19 | 3.36 | 3.01 |
| 22:45 | 1970 | Vitoria Setubal vs Casa Pia Atletico | 5.44 | 3.84 | 1.53 |
| 23:00 | 1764 | Fulham vs Chelsea | 3.22 | 3.37 | 2.12 |
| 23:00 | 3565 | Roma vs Genoa | 1.43 | 4.37 | 6.76 |

IJUMAA - 13/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 4156 | Cordino MA vs Moto Clube MA | 3.80 | 3.10 | 2.06 |
| 01:15 | 4192 | Bahia De Feira BA vs Vitoria BA | 3.47 | 2.88 | 2.15 |
| 01:30 | 2604 | Gremio Anapolis GO vs Atletico GO | 5.65 | 2.97 | 1.70 |
| 02:00 | 1624 | Univ de Chile vs Talleres | 2.77 | 3.31 | 2.29 |
| 03:30 | 1083 | Flamengo vs Audax Rio EC RJ | 1.39 | 4.26 | 6.97 |
| 04:00 | 1962 | Zacatepec vs Alacranes de Durango | 1.73 | 3.54 | 4.18 |
| 06:00 | 2820 | Club Atlas vs Monarcas Morelia | 1.94 | 3.39 | 3.79 |
| 11:45 | 3929 | Macarthur FC vs Central Coast Mariners | 3.04 | 3.53 | 2.16 |
| 17:00 | 2424 | Kayserispor vs Sivasspor | 2.28 | 3.38 | 2.94 |
| 18:00 | 1407 | Qatar vs United Arab Emirates | 2.05 | 2.96 | 3.64 |
| 18:00 | 4719 | Farco FC vs Ceramica Cleopatra | 4.00 | 2.95 | 2.06 |
| 20:00 | 1179 | Ismaily SC vs Arab Contractors | 2.79 | 2.74 | 2.84 |
| 20:00 | 4464 | Galatasaray vs Hatayspor | 1.28 | 5.57 | 8.56 |
| 20:30 | 4817 | Amazulu vs Kaizer Chiefs | 2.80 | 3.00 | 2.65 |
| 21:00 | 4641 | Algeria vs Libya | 1.50 | 3.94 | 6.78 |
| 22:45 | 5758 | Napoli vs Juventus | 1.92 | 3.37 | 3.82 |
| 23:00 | 3608 | Celta Vigo vs Villarreal | 2.77 | 3.22 | 2.51 |
| 23:00 | 4241 | Aston Villa vs Leeds | 1.92 | 3.48 | 3.68 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Alhamisi Januari 12, 2023
Nipashe



UKURASA 21

## Ten Hag ajipanga kuipa United taji



Mshambuliaji wa Simba Queens, Oppa Clement (kushoto), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Mkwawa Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mkwawa, mkoani Iringa jana. Simba Queens ilipata ushindi wa mabao 2-0.**PICHA: SIMBA SC**

# FEI TOTO AGOMA KURUDI JANGWANI

●●●Mikakati ya kukata rufaa CAS yaanza, aeleza hana mpango wa...

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Yanga kinaingia kambini leo, kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto' anajipanga kupeleka malalamiko yake katika Mahakama ya Usuluhishi ya Michezo ya Kimataifa (CAF), kupinga uamuzi wa yeye kurejeshwa kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Fei Toto kwa sasa yuko visiwani hapa akifanya mazoezi na timu yake ya zamani ya JKU ili kulinda kiwango chake.

Mwanasheria wa kiungo huyo, Salum Nduruma, alisema mteja wake amefikia uamuzi huo baada ya kutoridhishwa na hukumu iliyotolewa na Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Nduruma alisema Fei Toto anataka uamuzi wake wa kuvunja mkataba wa Yanga uheshimiwe kwa sababu amefuata mwongozo katika kusitisha huduma yake ndani ya klabu hiyo.

"Juzi (Jumatatu), tulipokea nakala kutoka TFF ambayo haina tofauti na maelezo yaliyotolewa hivi karibuni yanayosema mchezaji huyo ni mali ya Yanga, Fei Toto ameamua kusonga mbele kwa kuchukua hatua nyingine. Kwa sasa tunasubiri kupokea mwenendo yale yaliyoongelewa siku ya kusikilizwa baada ya hapo kwenda kama hataridhika, tutakwenda CAF kupinga hukumu hiyo," alisema Nduruma.

Mwanasheria huyo aliongeza mteja wake hana mpango wa kurudi kuichezea Yanga na anaona Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji haijamtendea haki katika shauri hilo.

Aliongeza Fei Toto bado hajapata timu mpya ya kuitumikia kwa sababu sakata lake linaendelea kufanyiwa kazi na analinda kiwango chake kwa kufanya mazoezi ya pamoja na JKU, klabu ambayo aliitumikia kabla ya kutua

INAENDELEA UK. 23

## Mgunda afunguka kuhusu Robertinho

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, amesema amefurahishwa na kuchaguliwa kuwa Kocha Bora wa Desemba ikiwa anapata tuzo hiyo kwa mara ya pili mfululizo lakini pia akiongeza amekuwa na wakati mzuri chini ya Kocha, Roberto Oliveira 'Robertinho'.

Akizungumza na gazeti hili kutoka Falme za Kiarabu, Dubai ambako Simba imeweka kambi, Mgunda alisema kwa muda mfupi aliokaa na Robertinho, kumekuwa na ushirikiano mkubwa katika kutimiza majukumu yao.

Mgunda alisema anaamini Robertinho atasaidia kuongeza mbinu ambazo zitasaidia timu kufanya vizuri na hatimaye kufikisha malengo yake.

"Mimi nimefurahi sana kufanya kazi na kocha huyu (Robertinho), kwanza ananiheshimu sana, pili tuko pamoja kwa kila kitu, ninachofurahi anajua kila klabu ina utamaduni wake, hivyo muda mwingi tunakuwa wote ili kuangalia nini tunafanya na ananiuliza mambo mbalimbali.

Kikubwa amenizidi, kwa hiyo mimi nachota mambo mengi kutoka kwake ambayo hapo mbele ya safari yanaweza kunisaidia, mtu anayekwambia eti sina furaha ni mwongo," alisema Mgunda.

Kuhusu tuzo aliyoipata alisema haitokani na uwezo wake peke yake, bali ni kwa kushirikiana na wachezaji, wanachama pamoja na mashabiki wa timu hiyo.

"Ni jambo la faraja wapo watu wanatambua unafanya nini, nawashukuru pia wachezaji wa Simba kwa sababu wamechukua kile nilichowafundisha kwenye mazoezi na kukipeleka uwanjani, benchi la ufundi kwa kunisaidia kazi kuwa rahisi, wanachana, wapenzi na mashabiki kwa sababu walikuwa karibu na wachezaji, walikuwa wanasafiri mikoani kila timu inapocheza," alisema Mgunda.

Kocha huyo aliongeza umoja na ushirikiano ulioko katika kikosi hicho pia unasaidia sana kuimarisha kikosi na si vinginevyo.

"Hapa kuna umoja na ushirikiano mkubwa ambao nimeupata tangu nilipojiunga na Simba, hiyo ndio siri iliyotufikisha hapa, si kwa nguvu zangu tu," alisema kocha huyo ambaye pia alikuwa kocha bora Novemba.

Mgunda pia amempongeza kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Clatous

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042